

MSIOGOPE, NI MIMI

 Hebu na tuendeleo tu kusimama kwa dakika moja na kuinamisha vichwa na mioyo yetu mbele za Mungu. Na huku tumeinamisha vichwa na mioyo yetu, sijui kama kunaweza kuwa na haja, usiku wa leo, ambazo ungetaka Mungu akukumbuke kwa—kwa namna *fulani* na kwa jambo *fulani*, kama kunazo, Mwinulie tu mkono wako namna *hiyo*. Sasa, Yeye anaelewa, anajua kila hatua, Yeye hana kikomo. Sasa, wekeni tu hilo niani mwenu tunapomba.

² Baba wa Mbinguni, tunahesabu haya kuwa moja ya majaliwa makuu kuliko yote maishani mwetu, ni kuja mbele ya Walionunuliwa na Damu Yako, Kanisa ambalo limezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu. Basi usiku wa leo, wakati tumekusanyika pamoja katika Jina la Bwana Yesu... Tuliambiwa na Yeye, ya kwamba popote wawili au zaidi walipokusanyika katika Jina Lake, Yeye angekuwa miongoni mwetu. Sasa, haina budi kuwa hivyo, Yeye aliahidi jambo hilo.

³ Na halafu tunafundishwa ya kwamba siku inapoanza kukaribia hata mwisho, kwamba tusiache kukusanyika, pamoja, kama wengine wasio na imani, bali inatupasa kukusanyika pamoja. Na tunafundishwa pia ya kwamba tumeketi katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, tukibatizwa katika Mwili Wake kwa Roho mmoja. Ndipo tuko pamoja Naye, tumefufuliwa pamoja Naye katika kufufuka Kwake, na katika Uwepo Wake, tukijua ya kwamba Yeye ni... daima yu hai apate kufanya maombezi, nasi tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili.

⁴ Na sasa usiku wa leo, Bwana, kulikuwa na mikono iliyoinuliwa, Wewe unajua kilichokuwa chini ya mkono huo moyoni, wanashikilia haja hiyo moyoni mwao sasa, Mungu, yasikie na kuwajibibia maombi. Tunakushukuru kwa sababu tuna ahadi, nayo ahadi... na imani ni hakikisho pamoja na ahadi hiyo kwamba watapewa. Okoa kila nafsi iliyopotea, Bwana, mrudishe kila aliyerudi nyuma, mponye kila mgonjwa, Bwana, ukipatie Mwenyewe utukufu.

⁵ Zilizowekwa mbele zetu hapa sasa ni lesu, vitambaa, Biblia. Sasa, tunafundishwa katika Biblia ya kwamba walichukua kutoka kwenye mwili wa Mtakatifu Paulo lesu na nguo, pepo wachafu wakawatoka watu, magonjwa yalikuwa, waliponywa. Sasa, tunajua ya kwamba sisi si Mtakatifu Paulo, bali Wewe ungali ni Mungu yeye yule, Yesu yeye yule.

⁶ Na pia, tuliambiwa wakati mmoja ambapo Israeli walikuwa njiani kwenda kwenye nchi ya ahadi, lile Kanisa kuu la Mungu lililoitwa litoke Misri, na njiani mwake, moja kwa moja kwenye wajibu wao, Bahari ya Shamu iliwakatilia mbali kutoka

nchini. Mungu akaangalia chini kupitia ile Nguzo ya Moto kwa macho yenye hasira, kitu fulani kilichokuwa kimesimama njiani mwa watoto Wake kuwazuia wasifikie ile ahadi, bahari ikaogopa, iliyafingirisha mawimbi yake na maji yake, nao Israeli wakavuka juu ya nchi kavu.

⁷ Sasa, Wewe ni Mungu yeye yule aliyekuwa pamoja na Musa, Nguzo ile ile ya Moto, Mungu yeye yule. Sasa, unapoziangalia ishara hizi, Bwana, zinapowekwa juu ya wagonjwa, Mungu, si kupitia ile Nguzo ya Moto, bali kupitia Damu ya Yesu uangalie chini na kujua ya kwamba kwa kupigwa Kwake waliponywa.

⁸ Nawe ulisema katika Neno lako, “Zaidi ya mambo yote nataka mfanikiwe katika afya.” Basi jalia nguvu za Shetani ambazo zimewakatilia mbali na hiyo afya njema, jalia aogope na aondoke, na jalia wavuke waingie kwenye nchi hiyo ya afya na nguvu, na kuishi kwa furaha hapa, wakimtumikia Mungu. Tujalie, Bwana.

Njoo usiku wa leo kwa nguvu kuu, utushukie tunapoinyenyekeza mioyo yetu mbele Zako. Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba. Amina.

⁹ Mwaweza kuketi. Bwana awabariki daima. Ndio kwanza nisikie rasmi, alasiri ya leo, kuhusu kiamshakinywa cha wahudumu asubuhi, nami nina furaha kwa ajili ya nafasi hii kupata kukutana na ndugu na kufanya ushirika. Mwajua, kuna kitu kuhusu kula kinacholeta ushirika. Sijui ni kwa nini, bali ina—inafanya tu; inaleta ushirika.

¹⁰ Nayo Biblia inatwambia, ya kwamba wakati Yesu alipokuwa karibu kuondoka kutoka maisha haya kuingia katika milki za Milele za waliobarikiwa, alitaka kula pamoja na wanafunzi Wake, Naye akachagua chumba kwa unabii Wake, kasema, “Enendeni sasa mjini, nanyi mtamkuta mtu akiwa na jagi la maji, mkamfuate. Na popote aendapo, mwambieni mwenye nyumba ya kwamba mnataka kukipangisha hicho chumba.” Na kwa hiyo, akakusanyika pamoja nao kupata... kula mkate, na kunywa divai, na—na kufanya ushirika kabla ya kuondoka Kwake.

¹¹ Nasi tunajisikia hivyo pamoja na ndugu zetu. Tunapoingia mjini, karibu tu na wakati wetu wa kuondoka, tunapenda kufanya ushirika sisi kwa sisi, kuzungumza na—na kuonyesha hisia zetu na shukrani sisi kwa sisi, na kuombeana, kwani kwa kweli, tuko vitani, na tunahitajiana kuliko tulivyowahi kuhitajiana katika nyakati zote. Tunahitaji... Wakristo, tunahitajiana sasa kuliko wakati wowote.

Sasa, sisi, tuna imani ya kwamba Mungu hujibu maombi na kutupa baraka Zake.

¹² Na sasa, kesho usiku, Bwana akipenda, ningetaka kuzungumza juu ya ujumbe wa wokovu kwa kanisa, kwa watu. Waleteni wale wasio na Kristo na wale waliorudi nyuma, na

hebu tuzungumze nao kuhusu—kuhusu Mungu kesho usiku, na jinsi ya kumrudia Kristo.

¹³ Wengi wameshikilia kadi za maombi, nasi tutamwombea kila mgonjwa ambaye anataka kuombewa kabla hatujaondoka mjini, kama itatubidi kukaa hapa mwezi mmoja kufanya hivyo. Mnaona? Tunaninii... hilo ndilo lililotuleta hapa, kwa hiyo tutamwombea kila mtu anayetaka kuombewa. Naye Mungu atafanya njia, nasi tuta—tutaichukua. Sisi... kama tu... tunaenda tu jinsi tunavyojisikia kuongozwa kwenda, na kwa hiyo, hilo daima ndilo bora zaidi.

¹⁴ Tulifanya jumbe zetu kuwa rahisi sana, kwa njia ya kitoto, kamwe hatukuuendea kwa undani, kwa njia ya kitheolojia, kwa sababu hii ndiyo mara yetu ya kwanza hapa. Hatuwataki muukose huu Ujumbe, tunataka kuufanya hivi kwamba watoto wadogo wauelewe, mchezo mdogo wa kuigiza, lakini hata hivyo, ni Maandiko kabisa. Na kama... Ni kweli. Ninii tu...

¹⁵ Lakini sasa, wakati tungezungumza na makasisi, tungezungumza nao katika kitengo cha juu zaidi, tuliendee kwa njia nyingine, ama—ama watakatifu ambao wameiona huduma na wamekuwa karibu nayo, na wanajua jinsi gani, tungeingia kwenye kitengo cha juu zaidi. Lakini hapa tulijaribu kulifanya rahisi tu, ili kwamba hakuna mtu atakayelikosa. Nami nilihisi Roho Mtakatifu akiniambia hivyo, ku—kufanya hivyo wakati nikiwa hapa katika—katika hii Santa Maria.

¹⁶ Na mimi—mimi... ninatumaini ya kwamba baada ya kuondoka, ya kwamba kutakuwako, kutoka hapa, kwamba kutakuwako na uamsho mkubwa sana miongoni mwa makanisa! Na—naomba tu ya kwamba Mungu atawabariki sana na kuwafanya tu nu—nu—nuru kwa ulimwengu wote, papa hapa Santa Maria, na watu hawa wote wazuri, na wa madhehebu yote, mnaona.

¹⁷ Sisi sote ni wanadamu, sote tunakula chakula cha aina ile ile, sote tunawapenda wake zetu na watoto wetu; sisi ni—sisi ni wanadamu ambao Kristo aliwafia. Wakati mwingine umadhehebu umetukatilia mbali kidogo, lakini sisi ni... hakika katika Uwepo wa Mungu, tunaweza kuangalia juu ya hizo kuta ndogo hapo, na kuwaona ndugu zetu ng'ambo ya pili, na tulitandaze hema letu mbele kidogo, na kumkaribisha ndani pia, mnaona, maana hivyo ndivyo tunavyotaka kumfanyia kila mwanadamu.

¹⁸ Kristo alikufa apate kumwoko kila mtu aliyepotea, haidhuru kanuni ya imani imewafanyia nini. Hiyo daima imejaribu kuwa njia yangu ya ku—kuwaendea watu, ni kuwa mtumishi wa umma wa Kristo kwa “yeyote atakaye,” mnaona. Kwa yeyote yule, niko hapa kutumika. Yeye hajawahi kuweka mpaka kwa mtu yeyote nitakayemwombea. Kamwe hakusema, “Sasa, hawa ni Wamethodisti, usiwaombe; hawa ni Wakatoliki,

usiwaombee.” Yeye alisema tu, “Waombee watoto wagonjwa.” Kwa hiyo hilo—ni hilo tu. Kwa hiyo wao ni—wao ni... Nami ninataka tu kuninii... Hivyo ndivyo ninavyolifanya.

¹⁹ Hiyo ndiyo sababu siungi mkono yeyote. Ninaamini tu Neno na kudumu tu moja kwa moja na Neno. Na mtu yeyote mwenye akili timamu atajua ya kwamba Neno hilo ni kweli. Halina budi kuwa sawa, mnaona. Nami siliwekei tafsiri yoyote, ninajaribu, kulisoma tu jinsi linavyosema, kisha nasema jambo lile lile; hayo ni maungamo.

²⁰ *Kuungama* linamaanisha “kitu kile kile,” kama vile, “Yeye ni Kuhani Mkuu wa,” vema, toleo la King James linaliweka “maungamo” yetu. Lakini *kuungama* na *kukiri* ni jambo lile lile, mnaona. Kwa hiyo basi *kukiri*, hilo linamaanisha “kusema jambo lile lile alilosema Yeye.” Kwa kupigwa Kwake nimeponywa; ninakiri. Mnaona? Ninakiri jambo lile lile alilosema. Mnaona? Ninafanya maungamo.

²¹ Hivyo ndivyo ilivyo mahakamani, inakubidi kusema jambo lile lile. Sasa niko, kwa Kuhani wangu Mkuu, kwa maana Yeye ameketi mkono wa kuume wa Ukuu kufanya maombezi ninapokiri. Kwa hiyo mnaona, kabla Mungu hajakufanyia lolote, inakubidi kwanza kuliadini na kulikiri, Hawezi kufanya kazi, hawezi kufanya jambo moja.

²² Nawaambia, si ajabu watu wanaogopa uponyaji wa Kiungu. Ninasema hili kwa uchaji na udugu, lakini kumekuwa na udanganyifu mwingi sana unaoitwa uponyaji wa Kiungu, mnaona, ambao umewaogopesha watu. Kumbukeni tu, sanamu ya kutishia ndege iko wapi? Chini ya mtofaa ulio bora zaidi. Hiyo ni kweli. Daima ni tikiti ya posho. Ukitaka kujua mahali matofaa yaliyo bora sana yalipo kwenye shamba la matunda, tafuta tu ambapo marungu yote, na vijiti, na sanamu za kutishia ndege, na kadhalika vilipo, wanajaribu kuwazuia wasiukaribie mti huo. Na hivyo ndivyo ibilisi afanyavyo hasa.

²³ Ninakumbuka wakati mmoja, miaka kadhaa iliyopita, nilipata somo juu ya jambo hilo. Ni wangapi wanaojua bukuardhini ni kitu gani? Kwani mnatoka sehemu gani ya Kentucky? Nilikuwa... Kulikuwa na maskini shimo la kuzamia, nami nilikuwa nimepanda ninii... Sasa, kwa kweli ni ninii... Jina lake ni panyabuku, bali tunamwita bukuardhini. Yeye ni—yeye kweli ni Mmarekani, kwa sababu yuko kote nchini. Naye ni maskini mnyama mzuri, maskini mla mboga. Naye ni jamaa mdogo katili pia.

²⁴ Kwa hiyo siku moja nilikuwa nikipanda maharagwe manjano, na kwa hiyo, nilipandia maharagwe manjano haya, nisingeweza kuyakuza, maskini bukuardhini huyo mdogo angeshuka moja kwa moja kwenye safu, akayala yote, kisha akarudi shimoni mwake, akaketi huko nyuma, nadhani, na

kuchokoa meno yake, kisha kuniangalia. Kwa hiyo nikawazia, “Nitamshitusha jamaa huyo vibaya sana.”

²⁵ Kwa hiyo kusema kweli, mimi...mke wangu, aliyeketi hapa, angeweza kuwaambia mimi ni mwanasanaa kweli kweli, mwajua. Kwa hiyo nikajichorea picha ya uso mkubwa wa kutisha. Na chochote ambacho ningechora hata hivyo kingekuwa cha kutisha sana. Kwa hiyo ni—nikacho... (Asante, Ndugu.) Nikachora picha ya uso huu mkubwa mno na kuweka maharagwe manjano kwenye gunia, na kulifunga, nikashindilia kijiti ardhini, nikakiweka pale juu, na—na kwa hiyo, nikakiweka papo hapo kwenye safu ambamo maharagwe yangu ya manjano yalipandwa.

²⁶ Kutoka shimoni akaja maskini yule bukuardhini. Nami nikarudi kule na kuangalia kupitia darubini yangu kumchungulia. akatoka mle na kuangalia pande zote, aone kama nilikuwa mahali popote, naye hakuniona, kwa hiyo akaanza kula maharagwe manjano, moja kwa moja akalikaribia gunia hilo. Ilikuwa ni siku tulivu, upepo haukuwa ukivuma.

²⁷ Kwa hiyo akasimama, maskini jamaa huyo, akasimama, kisha akaliangalia lile gunia. Akainuka kwa maskini miguu yake ya nyuma na kugeuka upande na kuliangalia, *hivi*. Naye a—alijua kulikuwa na kitu fulani, huo uso mkubwa wenye sura mbaya juu yake. Naye akasogea karibu sana, mwajua, naye akalirukia mara nne ama tano aone kama lingeruka, kamwe halikusogea.

²⁸ Kwa hiyo akalipiga kwa unyayo wake mdogo, nalo likayachacharisha hayo maharagwe manjano, akaruka nyuma hatua nne ama tano, kisha akaliangalia tena, akalipima tena, na kulipiga tena, nao uso huo wa kuchukiza, likachacharika tena. Kisha akaanza kuutikisa kwa unyayo wake. Ilikuwa ni kuchacharika tu, kwa hiyo akalizunguka moja kwa moja huko nyuma yake na kuanza kula hayo maharagwe manjano; halikumsumbua hata kidogo. Mnaona?

²⁹ Unapooni kitu ambacho ni bandia, usikijali, zunguka moja kwa moja nyuma yake na uendele kula. Hivyo tu. Unaona? Unaona? Usiache chochote kikutishe. Mungu ni Mponyaji, daima amekuwa, daima atakuwa.

³⁰ Na sasa, usiangalie miujiza. Usimwambie Mungu jinsi unavyolitaka, wewe likubali tu jinsi anavyokupa. Wewe shika tu ahadi Yake na uishikilie. Sasa, hilo limekuwa ndilo kusudi langu, hilo ndilo nimekuwa nikijaribu kuelezea mbele ya hili—hili kanisa hapa Santa Maria, ni kumkubali Yeye kwa kuamini tu Neno Lake katika matendo. Mnaona? Uwepo na dhihirisho la Kristo, halafu basi, kubali sio tu uponyaji, bali kila ahadi aliyotoa, kwa ajili ya Roho Mtakatifu, kwa ajili ya chochote. Likubali juu ya msingi kwamba Uwepo Wake upo hapa kuthibitisha ahadi Yake.

³¹ Sasa, mwajua, hiyo kweli ndiyo njia ya Mataifa ya kumpokea Kristo. Mnajua, kulikuwa na Myahudi, wakati mmoja katika Biblia, aliyesema, “Binti yangu ni mgonjwa sana, yuko karibu kufa. Njoo, weka mikono Yako juu yake naye atapona.” Mnaona? Sasa, maskini Yairo, kwa hiyo sikuzote nilimhurumia, kwa namna fulani alikuwa ni mwaminio wa kisiri. Basi wakati... Baadhi—baadhi ya watu, mwajua, ambao hawaamini katika uponyaji wa Kiungu, bali acha mtu akaribie kufa, naye daktari awakatae, ndipo wanaamini upesi sana katika uponyaji wa Kiungu, mnaona. Kweli hujawa mgonjwa vya kutosha bado, hivyo tu.

³² Lakini wakati...alifikia mahali mtoto wake wa pekee alikuwa amelala akifa, ndipo akaenda kumtafuta Yesu. Sasa, mwangalieni, yeye alikuwa ni Myahudi: “Njoo, weka mikono Yako juu ya binti yangu, naye atakuwa mzima.” Sasa, huyo alikuwa ni Myahudi.

³³ Mwangalieni Mmataifa, Mrumi: “Sistahili Wewe uingie chini ya paa langu.” Mnaona? “Sema tu Neno, na mtumishi wangu ataishi.” Hiyo ndiyo tofauti, mnaona.

Sasa, tunapaswa kumwamini Mungu, ndipo Yesu akageuka, mnakumbuka lile tamshi Lake kuu? “Sijaona imani kama hiyo katika Israeli.” Mnaona?

“Nena tu Neno, mtumishi wangu ataishi.”

³⁴ Nilikuwa nikizungumza jana usiku juu ya yule mwanamke, maskini malkia wa Sheba, kama tumjuavyo siku hizi, Yesu alimwita malkia wa Kusini, naye aliishi katika sehemu za mwisho kabisa za ulimwengu uliojulikana wa siku hizo. Nami kwa namna fulani nilikikemea kizazi hiki kwa kutokuupokea, na jinsi ambavyo umeenea kote nchini, na—na kadhalika, nao wangali hawaupokei. Nami nikasema jinsi ambavyo watu hawatavuka barabara sasa.

³⁵ Leo nilikuwa nikichunguza pande zote, nami nikaona kuna watu hapa kutoka mbali sana. Hiyo inaonyesha ya kwamba baadhi yao wanatoka mbali sana. Sasa ninawaangalia mume na mke, Bw. na Bibi Tom Simpson, wanatoka Saskatchewan, Canada, wapate kuwa mkutanoni. Ndugu Tom, waweza kusimama tu? *Hapa*. Kutoka Saskatchewan, Canada, yeye na familia yake.

³⁶ Nyuma yake tu ni Ndugu Fred Sothmann, mkewe na familia yake. Wao pia, sasa hivi wako Jeffersonville, watu hawa, lakini yeye anatoka Rosetown, Saskatchewan. Waweza kusimama, Ndugu Sothmann, ninii tu...? Yeye, kutoka Rosetown, na hiyo ni kutoka mbali sana.

³⁷ Dada Ungren, Dada Downing, binti yake, naye ana binti wawili hapa, na mjukuu wa kike, kote kutoka Memphis, Tennessee. Sijaona...Nilimwona huyo binti mtaani leo. Je, waweza kusimama, popote ulipo, Dada Downing, ama Dada

Ungren, kutoka Memphis, Tennessee? Uko wapi, usiku wa leo? *Pale*. Nina furaha sana kuwa nanyi nyote mkutanoni.

³⁸ Pia kuna marafiki zangu mkutanoni, Ndugu na Dada Welch Evans kutoka mbali huko Tifton, Georgia, yapata maili elfu tatu kote nchini, na familia yao. Mwaweza kusimama, Ndugu Evans, na Dada Evans, familia yako hapa? Basi tuna furaha kuwa nao pamoja nasi, kutoka mbali huko Tifton, Georgia.

³⁹ Ndugu Willie, ninasahau jina lake, ninaamini ametoka mbali sana kutoka Tifton pia. Nilimwona hivi majuzi hapa. Yeye yuko hapa kutoka Tifton, Georgia, na kwa hiyo tuna furaha sana kuwa nao hapa.

⁴⁰ Ndugu na Dada Wood kutoka Jeffersonville, Indiana, wako hapa pia. Yuko wapi Ndugu Wood ama Dada Wood, usiku wa leo? Ndugu Wood na Dada Wood kutoka Jeffersonville. Hao walikuwa watu ambao Bwana alifanya jambo kubwa sana, walikuwa na mvulana aliyelemaa kutokana na polio, akiwa na mguu uliokunjamana. Ndugu Wood alikuwa ni Shahidi wa Yehova, na kwa hiyo, baba yake alikuwa msomaji katika shirika la Mashahidi wa Yehova.

⁴¹ Naye akasikia habari zake, nao wakashuka wakaja Louisville, Kentucky. Ndipo msichana mmoja alikuwa mkutanoni usiku huo, alikuwa akigeuka jiwe mpaka kwenye kiuno chake, daktari akasema, “Mikono yako yote imekwisha na kadhalika.” Kisha kesho yake usiku alikuwa akikimbia huku na huko kwenye vipandio, namna *hiyo*, kwa utukufu wa Mungu. Walidhani hilo linapaswa kutumika kwa mwana wao mwenye *polio*, nao... Nikaenda ng’ambo mara moja... Vema, walishuka kwenda Houston, Texas, ambako ile picha ya Malaika wa Bwana ilipigiwa, kwa uhalisi, nayo ikachunguzwa na George J. Lacy.

⁴² Wakati Mkatoliki akisimama pale akijadili, huku mhudumu Mbaptisti akisema hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu, na kadhalika, akijaribu kuanzisha mjadala, ama kujaribu kufanya hivyo na Bw. Bosworth.

⁴³ Nami nikasema, “Mimi sidai kuwa mungu, sidai kuwa mponyaji, ni—ninadai kuwa mtumishi wa Kristo. Kama mimi... Ninasema tu kama huduma hii inatiliwa shaka, Mungu na ajishuhudie Mwenyewe.”

⁴⁴ Nayo Hii hapa ikaja ikizunguka kote mkutanoni mbele ya maelfu mara maelfu ya watu, nao *wakosoaji* wakaipiga picha. Ilitumwa Washington, DC, usiku uo huo, negativu, na—nayo ikapewa hatimiliki kisha ikarudishwa. Tunayo, usiku wa leo, imepewa hatimiliki na Studio za Douglas huko Houston, Texas.

⁴⁵ Bw. Ayers, Mkatoliki wa Kirumi, alishikwa na mshtuko wa moyo usiku huo maana alikosoa, na kusema kwamba (Mwanamke aliyekuwa na tezi kooni mwake.), akasema ya kwamba nilimfanyia hiponozi tezi ikatoka kooni mwake, na vitu kama hivyo.

⁴⁶ Na—naye Bw. Kipperman, Myahudi wa kiothodoksi, pia alikuwa amesema mambo maovu, kisha akawa Mkristo hodari kwa sababu ya mwujiza huo. Nao umeenda kote ulimwenguni sasa.

⁴⁷ Bw. Wood alikuwapo. Mara baada ya hapo nikaenda ng'ambo, nikarudi. Alimleta mwanawe mlemavu huko, huko Ohio, Cleveland, Ohio. Ndipo usiku mmoja mkutanoni, kasema, "Roho Mtakatifu ananionyesha mvulana mdogo, mahali *fulani*, ambaye ana mguu uliolemaa, na BWANA ASEMA HIVI, ameponywa." Ndipo huyo kijana akaponywa mara moja, na sasa yuko pamoja nasi usiku wa leo, ameo na ana watoto wawili. David, uko karibu? David Wood, uko kwenye...? Huyu hapa, papa hapa pamoja na...La. Hata sijui ni mguu gani uliodhuriwa.

⁴⁸ Ndipo, baba yake, akiwa m—mkandarasi mashuhuri kote nchini, akauza kila kitu alichokuwa nacho, akapangisha nyumba alizokuwa amejenga, na kuhama akawa jirani yangu, naye ameishi hapo tangu wakati huo. Tangu wakati huo, mkewe, akiwa Mmethodisti, ama ilikuwa ni Church of God, na watu wake wote Wamethodisti, kila mmoja wa watu wake, kadiri ni juavyo mimi, amempokea Roho Mtakatifu na kujazwa na Roho wa Mungu tangu wakati huo.

⁴⁹ Kakake Bw. Wood alikuja akiwa mkosoaji, naye alikuwa... Roho Mtakatifu aliwafunulia kwa ono watu hao wote, na kuwaambia mambo kama hayo, akawasadikisha, ndugu zake, dada zake. Naye baba yake, msomaji, akashuka kuja kunikemea kwelikweli, ndipo Roho Mtakatifu akanena na kusema yale yangetukia kesho yake, Neno kwa Neno yakatimia. Alijazwa na Roho Mtakatifu na akapata ushindi, Bw. Wood. Loo, ingeweza kuendelea na kuendelea! Wengi hapa ambao mimi ni... Natumaini sitamkosa mtu yeyote, lakini kuna wengi hapa nina hakika ya kwamba tayari nimekuwa nikiwazia mawazoni mwangu, ama kwamba nilitaka kuwatambulisha usiku wa leo.

⁵⁰ Nitafanya jambo fulani, nitakemewa sana nitakapofika nyumbani. Malkia wangu, waweza kusimama, Mpenzi? Loo, najua uso wake ni mwekundu, lakini... Kamwe hapendi kufanya hivyo. Mke wangu, Bibi Branham. Na binti yangu mdogo, Sarah. Uko wapi, Sarah? Simama. Nafikiri yuko mkutanoni. Mwanangu mdogo, Joseph, yuko wapi? Simama, Joseph. Huyu ni mwanangu, Joseph. Nina mmoja zaidi ambaye hayuko hapa usiku wa leo, Rebekah.

Na naam, Ndugu Jim Maguire, mvulana wetu wa kanda, aliyeoa katika familia ya akina Sothmann, ndiye mvulana wa kanda anayesimama *hapa* kando.

⁵¹ Ndugu Welch Evans, hilo linanijia akilini, kwamba Ndugu Evans... Mara ya kwanza nilipokutana na Ndugu Evans... Natumaini sichukui muda mwingi kupita kiasi. Lakini Ndugu

Welch Evans, hivi nilimsimamisha muda mfupi uliopita (naamini nilimsimamisha.), yeye na familia yake?

⁵² Tulikuwa huko Philadelphia kwenye—kwenye mkutano, na baadhi...mvulana wa kanda, mmojawapo, Bw. Mercier, ambaye yeye ni...Ndugu Mercier na Ndugu Goad wameninii—wameninii...hawako pamoja nasi tena, wameingia katika kazi za kilimwengu, wala hawako kwenye miamsho tena.

⁵³ Naye Ndugu Mercier alikuwa amesema, “Kuna mtu kutoka kusini, jina lake Evans, anataka kukutana nawe.” Nami nikasema...“Je, mtakula kiamshakinywa pamoja naye asubuhi?” Naye alikuwa akishughulikia mambo hayo wakati huo, miadi na kadhalika, kama vile mwanangu anavyofanya sasa, Billy Paul.

Nami nikasema, “Naam, ingekuwa sawa.”

Akasema, “Alitaka kukutana nawe.”

⁵⁴ Mke alikuwa pamoja nami kwenye mkutano huu pamoja na mtoto Joseph, hiyo imekuwa yapata miaka mitatu iliyopita. Na ninyi nyote mnajua hadithi hiyo, au labda mmesoma habari za Joseph. Nilikuwa nikiyaelezea maisha ya Yusufu. Naye daktari alikuwa ametwambia tusingeweza kupata watoto zaidi baada ya Rebekah kuzaliwa, kwa sababu alikuwa ni wa upasuaji, naye mke wangu asingeweza kupata mtoto mwingine.

⁵⁵ Nami nikaingia kwenye chumba kidogo huko Minneapolis, nami nilikuwa nikilia kule mbele za Bwana, ndipo ono likashuka na kusema, “Utampata mwana, nawe utamwita jina lake ‘Joseph.’” Na kwa hiyo, nikaanza kuwatangazia watu wote, na kwa hiyo, kisha nikangojea miaka minne.

Basi kila mtu akasema, “Vipi kuhusu ule unabii kuhusu Joseph?”

Nikasema, “Atakuwepo, msijali.”

⁵⁶ Ndipo tukajua ya kwamba, mke wangu alikuwa mja mzito tena, na kwa hiyo wakati alipozaliwa, alikuwa ni msichana, Sarah. Ndipo kila mtu akaanza kunicheka, kasema, mimi... “Ulimaanisha Josephine, sivyo?”

Nikasema, “La, nilimaanisha Joseph.”

Daktari akasema, “Bw. Branham,” kasema, “afadhali tufanye upasuaji kidogo hapa, kwa sababu mke wako hawezi, kamwe, kustahimili mtoto mwingine.”

⁵⁷ Nikasema, “Daktari, usithubutu kumgusa. Tutapata mwana, na jina lake ni Joseph.” Alikuna tu kichwa chake, na kufanya *hivyo*, kisha akaondoka.

Basi miaka mingine minne ikapita, ndipo siku moja tukaona kwamba alikuwa mja mzito tena. Baadhi yao wakasema, “Huyu ni Joseph?”

Nikasema, “Sijui, lakini . . .” Nikasema, “Sijui, lakini Joseph yuaja, maana Mungu hajaniambia jambo lolote ila lililo kweli.”

Na kwa hiyo, nikatoka nje, hospitalini na kumbusu alipoingia chumbani, chumba cha kujifungulia.

Dakika chache, nesi akashuka, akasema, “Kasisi Branham ni nani?”

Nikasema, “Mimi.”

Naye akasema, “Una mvulana mzuri wa ratili saba.”

Nikasema, “Joseph, Kipenzi, umechukua muda mrefu kufika hapa. Baba kwa namna fulani ana furaha kukuona!”

Akasema, “Ulimwita ‘Joseph.’”

Nikasema, “Hilo ndilo jina lake.”

⁵⁸ Na kwa hiyo, tulikuwa huko, huko Philadelphia, ndipo asubuhi hiyo nikaamka, nami nilikuwa nikiangalia chumbani, Nikasema, “Mpenzi, mtu tunayekusudiwa kukutana naye asubuhi ya leo amevunja sheria.” Nikasema, “Amekuwa akivua samaki, naye akashika gunia zima la samaki, wengi kupita kiasi. Nami nilimwona akiwaficha mara mbili au tatu kutoka kwa mlinzi wa wanyama.” Nanyi mnajua jinsi nilivyokuwa mlinzi wa wanyama kwa miaka kadhaa.

Nami nikasema, “Nilimwona akiwaficha hao samaki kutoka kwa mlinzi wa wanyama pori.” Nikasema, “Jamani, hapo palikuwa ni mahali pazuri sana alipokuwa akivua samaki, na samaki we—wengi sana.”

⁵⁹ Na kwa hiyo papo hapo maskini Joseph akasimama akaja kwangu, yapata umri wa miaka minne, naye akasema, “Baba, Da-Da,” ambalo alimaanisha David, “atapata ajali ya pikipiki.”

Nikasema, “Unamaanisha nini?”

⁶⁰ Alikuwa tayari ameniambia ono, akasema, “Mimi . . . nikiwa nimepanda baiskeli yangu ndogo ya magurudumu matatu huko nje kwenda kumwangalia maskini dada yangu, Sarah, akija barabarani.” Naye akasema . . . “Baba, hivi Mungu ana mkono?”

Nami nikasema, “Ndiyo.”

⁶¹ Kasema, “Niliona mkono kama wako tu,” namna *hiyo*, ukiwa na sijafu, kisha kasema, “ulikuwa umenishikilia moja kwa moja, kunizuia nisingie barabarani wakati nilipokuwa nikimngojea dada yangu.” Vema, kamwe hatukulitambua, mwajua, tukiishi tu jinsi tunavyoishi, na kumsikia akizungumza juu ya maono, kwa hiyo ningewazia labda maskini jamaa huyo, mwajua jinsi . . .

Kwa hiyo asubuhi hiyo alisema, “David atapata ajali ya pikipiki, atachuna mguu wake upande wa kulia.”

Ndipo nikasema, “Joseph, ndio kwanza uamke, Mwanangu, njoo hapa.” Nikasema, “Je, uliota hilo?”

Akasema, “La, Baba, nilimwona tu David akiipata.

⁶² Siku nne ama tano kuanzia hapo, David . . . Mvulana mmoja alikuja kutoka Louisville akiwa na pikipiki, alitaka David aiendeshe, akaiendesha njiani, ikamtupa, ikauchuna mguu wake wa kulia, sawasawa kabisa.

⁶³ Tukaenda kumwona Bw. Evans na mke wake mpendwa. Nami nikasema, “Ndugu Evans,” (Baada ya kukutana naye, nikazungumza naye.), Nikasema, “unaishi, huko chini mahali palipo na uvuvi mzuri sana wa samaki.” Nami nikasema, “Mimi ni mvuvi.”

Naye akasema, “Naam, ndiyo.”

⁶⁴ Nikasema, “Majuma machache yaliyopita ulikuwa ukivua samaki nawe ulikuwa na gunia lililojaa samaki, haramu.” Nami nikasema, “Ilikubidi kuwaficha karibu mara tatu kutoka kwa mlinzi wa wanyama pori.”

⁶⁵ Akaniangalia, akasema, “Hiyo ni kweli.” Naye akaniangalia, kwa namna fulani akatoa jasho kidogo, nami nikasema, “Kuna ombi moja tu: Je, utanipeleka mahali hapo niende kuvua samaki?”

Akasema, “Nitakupeleka.”

⁶⁶ Tulishuka kwenda, kuvua samaki, na ilikuwa ni huko Florida, huko chini kwenye hicho kinamisi kidogo na kadhalika. Nasi tukatembea kwenye vinamasi vya mamba huko nyuma, ambako alikuwa na ndugu aliyekuwa ameninii, miezi michache tu kabla ya hapo, aliyekuwa ameumwa na nyoka mchacharika.

⁶⁷ Sasa, mnafikiri mgongoalmasi wenu ni mbaya, hebu mwangalieni tu mmoja wa hao jamaa wadogo, wabaya kuliko mwendakando. Naye . . . Nao wanalala moja kwa moja juu ya maji na kukuuma. Huko Florida, wao wananinii tu, nyoka wananinii tu, wako tu kwenye safu.

⁶⁸ Na kwa hiyo, tulikuwa—tulikuwa na bastola, na fimbo, nasi tungerudi kupitia hizi, ambapo walikuwa wamechimba mtaro wa kuzolea taka kupitia ranchi ya ekari elfu kumi na saba, na kuwaingiza ng’ombe wake wa Brahman mle ndani, nao walikuwa wamevurugikiwa. Nasi, huko nyuma karibu na hao samaki wakubwa mno. Jamani, walikuwa wa kupendeza jinsi gani! Tulikuwa na fito za popa, tulikuwa tukiwakamata. Na kwa hiyo tungeyasogeza mayungiyungi namna *hiyo*, na kuangalia pande zote tukitafuta mamba, na nyoka, na kadhalika, kisha tusonge mbele majini.

⁶⁹ Ndipo tukapanda mahali ambapo ule mtaro wa kuzolea takataka, ama, mtaro wa taka ulikuwa umemwagilia u—uchafu. Nami nilikuwa nimeshika baadhi; samaki wakubwa sana niliowahi kuona! Nami nilikuwa na mmoja mkubwa mno, mdomo wake ulikuwa mkubwa *hivyo*, na maskini nyukibambi huyu mdogo asingekaa kinywani mwake, ingembidi

kumshikilia, naye angeweza kumtema, ama kumtupa nje, naye mdudu huyu akiruka juu ya maji, angemnyakua tena. Nilimshika mara tatu, hata nisingeweza kumshikilia.

Bw. Evans alikuwa amekunja miguu ya suruali yake, naye akaja pale, akasema, “Ndugu Branham, nilikuona ukimshika huyo mkubwa!”

⁷⁰ Nikasema, “Loo, jamani, yeye ni mzuri sana!” Ndipo, Ndugu Evans, sitawaambia ya kwamba ulimwachilia samaki wangu alasiri hiyo kwa bahati mbaya. Kwa hiyo nitaninii... Nilikuwa na lundo kubwa lililofungwa, la samaki wakubwa wazuri mno, naye akaanza kuwaokota na kuacha huo uzi upite, ndipo lundo zima lao likaponyoka. Kwa hiyo tulikuwa na kumi na mmoja wazuri sana, walipigwa picha usiku huo.

⁷¹ Kwa hiyo tulikuwa... Nilikuwa na samaki huyu, nami nikamjaribu tena, ndipo mwingine akampiga, nadhani samaki huyo alikuwa na uzito wa ratili kumi na mbili, kumi na nne, kwa hiyo, samaki mkubwa mwenye mdomo mkubwa. Naye huyu, alikuwa akipigapiga maji, nami nilikuwa nikijaribu kumshika namna *hiyo*, nikasema, “La, huyo siye.” Kwa hiyo ningemchosha, akiwa na uzito wa ratili saba ama nane, nami nilikuwa nimemweka kuelekea ufukoni, ambapo manyasi na kadhalika yalikuwa yamesimama, naye akasema, “Ngoja kidogo, Ndugu Branham, nitakushikia huyo.”

Nikasema, “Usijali, ninaweza kumwingiza ndani.”

⁷² Lakini akaruka tu majini huku miguu ya suruali yake ikiwa juu namna hiyo, ndipo mara aliporuka, akaruka nyuma tena. Nyoka mchacharisha wa ardhini akamwuma na... papo hapo kando ya kiganja na mguu. Vema, sijawahi kuona maumivu kama hayo kwa dakika chache. Karibu ikupoozeshe na kuifanya mifupa yako kuganda ndani yako.

⁷³ Nami hapo nilikuwa huko nyuma, naye Bw. Evans atakuwa na uzito wa karibu mia mbili. Basi kulazimika kumbeba mtu huyo kupitia kwenye kinamasi hicho mgongoni mwangu ndilo jambo pekee ambalo lingeweza kufanywa, kumpeleka nje kwenye gari, karibu umbali wa maili mbili, nakisia. Mbona, yeye, akishikilia tu meno yake pamoja! Ndipo nikaangalia, nikaona upana wa kama inchi moja ambapo, sio ukubwa huo, ambapo haya, meno yote mawili yalikuwa yameuma papo napo miguuni mwake.

⁷⁴ Naye ndugu yake alikuwa akitembea kwa pete chini ya miguu yake, ambapo si zaidi ya yadi mia mbili kutoka hapo, alikuwa amemwua na nyoka mchacharika. Sasa, ndugu yake si Mkristo na angeninii... alilazwa hospitalini kwa sijui ni siku ngapi ama majuma mangapi. Na bado baada ya miezi kadhaa alikuwa na pete, akitembea juu yake, kwa muda mrefu.

⁷⁵ Naye huyu nyoka mchacharika alikuwa amemwua Ndugu Evans. Na mara tu niliponinii... nikawazia, “Ee Mungu,

tufanye nini?” Ndipo Andiko hili likanijia niani mwangu: “Watavikanyaga vichwa vya nge na nyoka, wala hakuna kitu kitakachowadhuru.” Ndipo nikaweka mkono wangu juu yake, Nikasema, “Baba wa Mbinguni, tuko katika hali ya dharura. Nawe ni Msaada uonekanao tele wakati wa mateso.” Mnaona? “Nawe umesema ya kwamba hakuna kitu kitakachowadhuru waaminio hawa, naye ndugu huyu ni mwaminio. Nami ninaomba rehema Yako.”

⁷⁶ Vema, maumivu yake yakakoma, ama, hayakuendelea, nilifikiri ilikuwa ni kwa minajili ya maombi yangu. Ndipo nilipomaliza, yeye akasema, “Hakuna maumivu mahali popote,” akasimama, tukaendelea kuvua samaki. Tulivua samaki siku nzima.

⁷⁷ Basi usiku huo, yapata saa tano tulikuwa tukiwaonyesha samaki hawa, ndipo ndugu yake akaja, naye alikuwa akimsimulia hayo. Ndipo ndugu yake mwenye dhambi akasema, “Welch, ni sawa kuwa wa kidini, lakini sio sawa kuingia kichaa.” Akasema, “Nenda hospitalini upesi uwezavyo, ukapate matibabu, la siyvyo utakuwa kama mimi.”

⁷⁸ Bw. Evans akamwambia, kasema, “Angalia, Ndugu, hayo yalitukia asubuhi ya leo yapata saa nne, naye Mungu ameniweka bila maumivu, na ni yapata saa nne usiku wa leo. Kama Mungu anaweza kuniweka umbali huo, Yeye anaweza kuniweka hata mwisho wa safari.” Kwa hiyo. . . Hiyo ni kweli, Bw. Evans? Uhm, ni kweli. “Wala wasingeweza kusema neno dhidi yake, mtu huyo alikuwa amesimama katikati ya watu.” Loo, Yeye angali ni Mungu, rafiki. Mnaona?

⁷⁹ Mtu huyo husafiri, yeye na familia yake, kila wakati ninapokuwa maskanini, na wakati mwingine hiyo ni juma baada ya juma, maili elfu moja mia tano kila Jumapili. Anakuja kwenye. . . anaanza Ijumaa na kufika huko Jumamosi, na kurudi Jumatatu au Jumanne. Naye ana kazi ya motokaa, nao wanasafiri umbali huo kuisikia Injili.

⁸⁰ Loo, mambo mengi sana yangeweza kusemwa! Nao huu hapa ni wakati, wa mimi kuanza kuwaombea wagonjwa, lakini ninachukua tu wakati huu, natumaini sikukatiza chochote, na ili tu kuwatambua baadhi ya watu ambao wamekuja umbali huu ku—kusikiliza. Sasa, laiti sisi sote, baada ya jambo hili, mara nyingine moja, tungeinamisha vichwa vyetu.

⁸¹ Baba yetu wa Mbinguni, mashahidi wa Injili wako karibu. Wewe daima uko karibu kusaidia na kuwabariki wale walio wahitaji. Nami nakuomba, Baba, ya kwamba Wewe utabariki na utawasaidia wale wote walio wahitaji. Nazo shuhuda hizi zinatolewa katika nuru ya Injili, ili watu walio wagonjwa na wahitaji wapate msaada na baraka kutoka kwa Injili.

⁸² Msaidie msichana huyu sasa, anayeteseka, hapa nyuma mkutanoni, kwenye wakati huu. Tunaomba ya kwamba rehema

Zako na neema zitakuwa juu ya huyu mama. Tujalie, Baba. Na jalia nguvu Zako ziwe zake, na umgawie baraka Zako.

⁸³ Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utatubariki sasa tunapolikaribia Neno la Mungu aliye hai, kwamba rehema na baraka kuu za Mungu zitakuwa juu yetu sote. Hawa wanashuhudia kwamba Wewe ni Mungu, na kwamba Wewe huna upendeleo, kwamba Wewe uko pamoja na wale wanaotamani, ku—kusaidia, na kutamani kuponywa. Kwa hiyo tujalie baraka hizi. Na tunaposoma Neno Lako tunaomba ya kwamba utalitia mafuta Neno Lako kwa manufaa ya wale wanaosikiliza. Katika Jina la Yesu, tunaomba. Amina.

⁸⁴ Sasa, katika Biblia, katika Mathayo mlango wa 14 kuanzia kifungu cha 22, ningependa kusoma. Na somo langu usiku wa leo ni, “Ushuhuda.”

Mara Yesu akawalazimisha wanafunzi wake wapande chomboni, na kutangulia mbele yake kwenda ng'ambo, wakati yeye alipokuwa akiwaaga makutano.

Naye alipokwisha kuwaaga makutano, alipanda mlimani faraghani, kwenda kuomba: na kulipokuwa . . . jioni alikuwako huko peke yake.

Na kile chombo kimekwisha kufika katikati ya bahari, kinatabika sana na mawimbi, kwa maana pepo zilikuwa za mbisho.

Hata wakati wa zamu ya nne ya usiku Yesu akawaendea, akienda kwa miguu juu ya bahari.

. . . wanafunzi walipomwona akienda juu ya bahari wakafadhaika, wakisema, Ni kivuli; wakupiga yowe kwa hofu.

Mara Yesu alinena nao, akawaambia, Jipeni moyo; ni mimi; msilogope.

Na Bwana na aongeze baraka Zake kwa hilo.

⁸⁵ Huyu mama ni mgonjwa? Mgonjwa sana. Vema. Wasemaje? Sasa, kila mtu, yale mliyofundishwa, kaeni kimya, inamisheni vichwa vyenu na mwombe. [Ndugu Branham anamwombea huyo mama, maneno hayatambuliki. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

⁸⁶ Sasa, msilogope. Iweni tu na kicho kabisa sasa. Mama mmoja amezimia, naye ni mgonjwa, nao watampeleka penye hewa. Tumemwombea. Nasi tunaninii. . . watampeleka penye hewa sasa, akapate hewa. Na sasa, hebu tuendeleo na . . . Imani haina hofu yoyote. Kwa hiyo iweni tu na kicho kabisa. Vema. Atakuwa sawa, ikiwa tu hamtatilia shaka sasa. Aminini.

⁸⁷ Sasa, tunapozungumza juu ya somo hili: *Msiogope, Ni Mimi*. Sasa, hapana shaka ilikuwa ni yapata wakati jua lilipotua jioni wakati yule mvuvi mashuhuri, mwenye nguvu, aliyejaa misuli

migumu mgongoni alipoanza kusogeza hicho chombo kutoka mchangani. Basi walipoanza kusogeza hicho chombo kutoka kwenye mchanga, wakageuza gubeti tena wakapanda juu, huku ameketi karibu na ndugu yake, Andrea, kwa kuwa walikuwa ni ndugu na wavuvi, na kuchukua kasia lake . . .

⁸⁸ Sasa, mashua za siku hizi si kama mashua za jana, zile mashua, wanazojiita meli, zilikuwa tofauti na meli zetu siku hizi. Tuna petroli, na mafuta, dizeli, na zinazotumia injini ya jeti, na . . . lakini siku hizo walienda tu kwa nguvu za mkono, ama kwa matanga katika upepo ndivyo walivyoiendea *hatima* yao pamoja na meli zao. Mara nyingi kulikuwa na dhoruba kubwa baharini, nao hawangeweza tu kumchukua mtu mmoja kwenye mashua, ilihitaji mikono yenye nguvu kushikilia mashua hizo.

⁸⁹ Ninyi watu hapa mnajua maana yake, huwezi kupandisha mashua moja kwa moja juu ya wimbi namna hiyo, utajizamisha mwenyewe. Huna budi kulitega wimbi hilo, ujue jinsi ya kulipiga kwa mashua yako kuipitisha kwenye dhoruba. Naye baharia hodari anaelewa jinsi ya kufanya jambo hilo, nao watu hawa hawana budi wawe mabaharia hodari la sivyo hawatapona.

⁹⁰ Na kwa hiyo walikuwa na kiti, nao wangemchukua mtu mmoja mwenye mikono miwili kwenye kasia kubwa upande *huru*, papo hapo upande wa pili kungekuwa na mtu mwingine mwenye makasia ya aina ile ile. Na wakati mwingine vifungo sita ama vinane vya makasia vingekuwa mle ndani, ambavyo vingezivuta mashua hizi kwa kazi ya pamoja; jinsi wangepanya, wakati ule ule, pigo lile lile! Nayo mashua hiyo ilipata msukumo mkubwa, pamoja na yale makasia makubwa yenye mabapa mapana waliyotumia siku hizo.

⁹¹ Basi huku kila mmoja akichukua mahali pake, wakayatumbukiza makasia yao majini, kisha wakaanza kuvuta mara mbili au tatu, kisha wanawapungia mikono watu waliokuwa ukingoni, “Kwaherini.”

Nao walikuwa wakisema, kama sikuzote tunapokuwa na mkutano mkubwa, “Rudini mkatuone.”

⁹² Kuna *jambo fulani* kuhusu wanadamu na Wakristo, wanapokusanyika pamoja katika nia moja na katika ushirika, wana mambo shirika. Unaweza kujua hi—hilo, jinsi wao . . . ni vigumu kwao kuachana.

⁹³ Na sasa, hili linaweza kuwa kando kidogo, lakini wengi wenu ninyi watu mmewaona watu ambao mnapenda tu kuwa walipo, halafu mmewaona watu ambao—ambao wewe . . . walikuwa ni watu wazuri lakini ilikuwa vigumu kwako kuwa walipo. Unaona? Wewe ni mwumbaji wa mazingira yanayokuzunguka. Na unayafanya hayo mwenyewe kwa tabia yako mwenyewe na roho iliyo ndani yako.

⁹⁴ Na kama tu vile maskini mama yangu mkusini alivyozoea kuniambia, ambaye ndio kwanza aende Mbinguni miezi

michache iliyopita, alizoea kusema, “Billy, Waswahili wa Pemba hujuana kwa vilemba.” Hiyo ni kweli. Kwa hiyo basi, kunguru, wala mizoga, na hua wasingeweza kuwa na ushirika mmoja na mwenzake, chakula chao ni tofauti. Mnaona? Hawawezi kula kitu kile kile.

⁹⁵ Na—na hivyo ndivyo ilivyo miongoni mwa Wakristo. Tunakusanyika namna hii, tunakusanyika pamoja, kwa sababu tuna mambo shirika. Tunapenda tu kuja mkutanoni. Mnapenda kumwona mchungaji wenu akipanda kwenye kipandio, nawe unapenda, maana unajua ataomba na kuheshimu nyumba yako, uwepo wake unamaanisha mengi sana kwako. Unataka kuwaleta watoto ndani, wakusanyike, kusudi baraka za mchungaji ziwe juu ya hao watoto. Na mnapotembeleana mnataka kusoma Biblia, na kuomba pamoja, kwa sababu mna mambo shirika.

⁹⁶ Loo, Kanisa linapaswa kuwa ndicho Kitu chenye utukufu kuliko vyote, ushirika huo! Jinsi ambavyo. . . Tulikuwa tukiimba maskanini, miaka mingi iliyopita, nilipokuwa mchungaji wa Maskani ya Baptisti ya Kimishenari, huko Jeffersonville, tulikuwa tukiimba ule wimbo wa kale:

Kibarikiwe kifungo kifungacho
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa watu wenye nia moja
Ni kama ule wa huko Juu.

Na tunapotengana,
Inatupa maumivu ya ndani;
Lakini bado tutaungana moyoni,
Na kutumaini kukutana tena.

Loo, hilo lilimaanisha. . . linatoka mioyoni mwetu. Tunapendana.

⁹⁷ Nao walikuwa wakishirikiana na Wakristo, watu wenye nia moja siku hiyo, nao wa—walikuwa na ushirika. Ndipo walipokuwa wakiondoka, wakivuka bahari, walikuwa wakipunga mkono, “Rudini, mkatuone tena. Njoni, mkatwambie juu ya Injili hii nzuri ya Uzima wa Milele, njoni pamoja na Bwana wenu,” wakipunga mkono, kisha mtu fulani angempigia mtu kelele, akisema, “Rudini,” labda jamaa.

⁹⁸ Nao wangepiga makasia mengine machache, na kupunga mkono, ndipo lile kundi dogo ukingoni likazidi kuwa dogo, dogo, na baada ya kitambo kidogo likafifia kabisa. Hapana shaka jua lilikuwa limetua wakati huo, nao walikuwa wakitaka kupumua mwajua, kwa sababu ya kutokwa na jasho kutokana na kupiga makasia hayo mazito. Iliwabidi kuvuka bahari usiku huo, ile Bahari ndogo ya Galilaya, nao walikuwa wamechoka kutokana na kazi ya siku hiyo, hapana shaka walisimama.

⁹⁹ Hapana shaka ilikuwa ni kijana Yohana, alikuwa ndiye mdogo kuliko wote, labda alichoka upesi kuliko hao mabaharia wenye nguvu. Kwa hiyo hapana shaka alisema, “Ndugu, hebu

na tusimame kwa dakika moja tu tupate kupumua.” Nami ninaweza kumwona wakati akipangusa jasho kutoka kwenye nywele zake zilizotimukatiimuka. “Whiu!” Akasema, “Mnajua, wakati tukipumzika kwa dakika chache,” wakati ile meli ndogo ilipokuwa ikifuata mkondo wake, hapana shaka Yohana aliinua kichwa chake na kusema, “ndugu zangu, ningetaka kutoa ushuhuda kidogo hapa.”

¹⁰⁰ Mwajua, daima kuna kitu fulani moyoni mwa mtu ambacho wanapenda kusema, kama wana, imani katika yale wanayosema. Kuna jambo fulani kulihusu, inakubidi kushuhudia na kusema jambo fulani.

¹⁰¹ Huenda Yohana alisema kitu kama hiki: “Tunaweza kuwa na hakika ya kwamba Mtu tunayemfuata si vile u—ulimwengu unavyomwita Yeye, nabii wa uongo. Yeye si Beelzebuli, kama makuhani wetu wasemavyo, mpiga ramli, Yeye si chochote pungufu ya Yehova.”

¹⁰² “Nilipokuwa mvulana mdogo tuliishi huko chini. . .” sasa, tunaingilia mkutano wa ushuhuda, “tuliishi huko chini karibu na Yordani. Nami ninaweza kukumbuka katika mwezi wa Aprili, wakati maua madogo yalipochipuka katika majira ya kuchipua, nilikuwa nikichuma maua haya madogo na kukimbia na konzi moja, na kumpa maskini mama yangu Myahudi mrembo. Naye angenipembeza alasiri mpaka nikashikwa na usingizi wangu, huko nje barazani, na kunisimulia hadithi za Biblia, nami ninazikumbuka nyingi sana.

¹⁰³ “Angeniambia habari za Yoshua, wakati alipowaleta wana wa Israeli chini kidogo tu ya kile kivuko huko, kutoka nyikani, nao wakavuka. . . moja kwa moja katika mwezi wa Aprili wakati Yordani ilipokuwa ikifurika, na huko juu kabisa kwenye kilele cha mto Mungu aliyashikilia maji, nao wakavuka moja kwa moja kwenye nchi kavu.

¹⁰⁴ “Na, hadithi zote, na moja iliniyokuwa ikinivutia sana ilikuwa ni ile aliyozoea kuniambia kuhusu watu wetu kuja kutoka Misri, ya kuja kwenye nchi ya uenyeji wetu ambayo Mungu alikuwa ametupa. Na jinsi Mungu alivyowajali walipoondoka Misri na kuanza kwenda kwenye nchi ya ahadi, jinsi Mungu alivyoahidi kuwapa kila kitu walichohitaji. Na jinsi ambavyo kila usiku, Mungu angeshusha mana, mkate, kutoka mbinguni na kuutandaza kote ardhini, na kesho yake asubuhi, jambo pekee lililowabidi watu wetu kufanya lilikuwa ni kutoka nje na kuokota mkate huu, na kuula, na kuishi siku nzima.

¹⁰⁵ “Nayo ilikuwa ikinishangaza kama mvulana mdogo,” huenda alisema, “Ningegeuka na kumwambia Mama, ‘Mama, Mungu aliupataje mkate huo? Kwani Yeye ana. . . Mbingu zote zimejaa tanuri kubwa kubwa, Naye ana kikosi cha usiku huko juu kinachofanya kazi, Naye huuoka mkate huu na kuwatuma

Malaika chini na kuutapanya kote ardhini kwa ajili ya watoto Wake?”

¹⁰⁶ “Akasema, ‘Sivyo, Yohana, mvulana wangu mdogo, huelewi, wewe bado ni mdogo sana. Si lazima Mungu awe na tanuri, Mungu ni Muumba, Yeye huumba tu mkate moja kwa moja kutoka hewani, nao unaanguka juu ya nchi, hivyo ndivyo anavyowalisha watu Wake.’

¹⁰⁷ “Basi ndugu, leo hii nilipomwona akichukua hizo biskuti tano na samaki wawili, na kuwalisha watu elfu tano, nilijua hana budi kuwa na uhusiano fulani na Yehova huyo, kwa sababu alikuwa ameumba mkate. Nilijua ya kwamba ilibidi kuwe na Muumba yule yule aliyeumba mkate huo wote nyikani, wakati yule mvulana mdogo aliyekuwa, aliyetoroka shuleni, na kutupatia chakula chake cha mchana. . . .”

¹⁰⁸ Sasa, mvulana huyo mdogo, ninataka kusema jambo fulani kwa wavulana hawa wadogo. Mnaona, mvulana huyo mdogo alikuwa na chakula kidogo cha mchana, hakikuwa kitu ila biskuti tano ndogo na samaki wawili wadogo. Sasa, maadamu mvulana huyo mdogo alikuwa nacho mkononi mwake, hakikumaanisha chochote, cha kutosha tu kujilisha, lakini alipomkabidhi Yesu hicho kidogo alichokuwa nacho, angalia kile kilichofanya. Sasa, huenda tukawa na kidogo tu, si kingi sana kwetu, bali kama tutamwacha tu Yesu akichukue, kile atakachofanya nacho! Aliwalisha watu elfu tano.

¹⁰⁹ Ninaweza kumsikia kijana Yohana akisema, “Mnajua nilichofanya? Nilipanda nyuma ya jiwe, nami nikamwona wakati alipoichukua biskuti hiyo na kuivunja na kuiweka kwenye sinia. Nami nikaangalia kila hatua moja kwa moja juu ya bega Lake. Na wakati alipounyoosha mkono Wake nyuma, alipoanza tena, kulikuwa tu na nusu biskuti, lakini wakati alipoenda kuweka mkono Wake juu yake, kulikuwa na biskuti nzima, naye akaimega na kuiweka chini tena.”

¹¹⁰ Ninataka kuwaulizeni, ndugu, Yeye aliachilia atomi ya namna gani hapo? Si ngano ya kulimwa na kuokwa, hatimaye, mkate, lakini tayari ilikuwa ni mkate, uliokwa; si samaki aliyepaswa kuuawa na kisha kukaangwa, bali tayari amekaangwa na yu tayari. Yeye alifanya nini?

¹¹¹ Inaonyesha kama—kama tuko tayari kuachilia kile kidogo tulicho nacho Kwake! Chukua tu imani uliyokuwa nayo ya kuja hapa usiku wa leo, na kuiweka mkononi Mwake na kudai uponyaji wako, na uondoke nao. Unaona? Angalia kitakachotukia.

¹¹² Kisha kasema, “Nilipoangalia jambo hilo, nilishawishika kabisa ya kwamba Huyu alikuwa ni Yehova. Ndipo nilipomtazama alipokuwa amesimama pale, bila kusisimkwa hata kidogo haidhuru ni kitu gani kilichokuwa kikiendelea, mtulivu tu awezavyo kuwa, akiuvunja huo, hata alionekana

kama Yehova kwangu aliposimama pale akiumega mkate huo na kuwasambazia watu hao wenye njaa.”

¹¹³ Akasema, “Sasa kwangu mimi, imetatuliwa milele kwamba Huyu ni Yehova. Na Yeye si, mwanadamu tu, Yeye si nabii tu, Yeye ni Mwana wa Mungu. Yeye ndiye Maskani ambayo Yehova anakaa ndani yake, kwa sababu Yeye aliumba mkate huu.”

¹¹⁴ Vema, huenda ilikuwa ni Simoni, mwajua, aliyejua jambo fulani kuhusu mambo hayo pia, aliyesimama na kusema, “Vema, hilo ni zuri sana, Yohana. Lakini kilichonisumbua kwanza wakati Andrea alipokuja, akaniambia kuna Nabii huko chini, vema, ilikuwa vigumu kwangu kuamini hilo. Lakini ninakumbuka baba yangu akiniambia ya kwamba ajapo Masihi atakuwa ni Nabii. Basi niliposhuka kwenda kule siku hiyo na . . . pamoja na Andrea, nami nikamwangelia usoni, basi Yeye aliniangalia na kusema, ‘Jina lako ni Simoni, wewe ni mwana wa Yona,’ hilo lilitosha kwangu milele. Nilijua huyo alikuwa ni Yeye, kwa sababu tumekuwa na miaka mia nne bila Nabii huyu na Huyu hapa anajitokeza. Nami najua ilikuwa ni majira, wakati ulikuwa sahihi, na huyo ilibidi awe Ndiye.”

Sasa, kumbukeni, Yesu hakufanya hivyo mara nne ama tano, Yeye alifanya hivyo mara moja, na hilo lilitosha. Walikuwa tayari; walijua ya kwamba Huyu alikuwa ni Yeye.

¹¹⁵ Huenda ilikuwa ni Filipo, wakati huo, aliyesimama na kusema, “Simoni, nilikuwa nimesimama pale. Ingawa mwujiza huo sikutendewa mimi, ulitendewa wewe, hata hivyo, niliamini, nami nikashawishika sana hata nikakimbia kuzunguka kile kilima nikamwona rafiki yangu hapa, Nathanaeli. Na wakati niliporudi na yeye, nilimwambia juu ya yale yaliyotukia, na yaliyokufanyikia, na jinsi tulivyojua ya kwamba hii ilikuwa ndiyo ishara ya Kristo, hivi ndivyo Maandiko yalivyosema alipaswa kufanya.

¹¹⁶ “Basia ulipokuja Mbele Zake, Yeye alikuangalia na kusema, ‘Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake.’ Nawe ukamwambia, ‘Rabi, ulipataje Wewe kunijua mimi?’ Naye akasema, ‘Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.’”

¹¹⁷ Basi huenda Nathanaeli aliruka juu wakati huo, kasema, “Na hilo lilitosha kwangu! Nikaanguka miguuni Pake, hapo alisimama kuhani wangu, na kuniangalia vibaya, lakini haikuleta tofauti yoyote aliendelea *kuangalia* jinsi gani, nilikuwa tayari nimeichunguza Biblia na kuona ya kwamba Huyu alikuwa ni Masihi. Kwa hiyo nikaanguka miguuni Pake na kusema, ‘Wewe ni Mwana wa Mungu, Wewe ni mfalme wa Israeli.’”

¹¹⁸ Loo, jamani! Hivi si ungetaka kuwa katika huo mkutano wa ushuhuda, umeketi hapo nje ukiyumbayumba katika maskini meli hiyo? Yapata wakati huo, labda—labda Nathanaeli alianza

kumsifu Bwana. Kisha kasema, “Keti chini. Unaitikisa meli. Ketu chini.” Mnajua.

¹¹⁹ Unajua, kuna jambo fulani kuhusu wakati unapoanza kusimulia juu ya wema wa Mungu, unafadhaika kabisa, unasisimkwa, unajua, mhemuko. Mtu fulani anasema, “Siamini dini yenye mhemuko.” Vema, afadhali uzike ulicho nacho, basi. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Kweli. Kwa hiyo kama dini yako haina mhemuko kidogo ndani yake, afadhali ukizike kitu hicho. Hiyo ni kweli.

¹²⁰ Nao hawana budi, walininii... maskini meli hiyo hapana shaka ilikuwa ikiyumbayumba vizuri sana wakati wote walipoanza kutoa ushuhuda. Na hapana shaka ilikuwa ni Andrea wakati huo, kamwe asingeweza kujizuia zaidi, kasema, “Ndugu, hebu kidogo, sote tunakumbuka huko chini Sikari siku hiyo, jinsi alivyotutuma mjini, na kununua chakula, naye alitaka kuachwa peke yake huko katika nchi hiyo ya Samaria. Alitwambia alikuwa na haja ya kupitia kule, Baba alikuwa akimtuma upande huo. Na kwa hiyo sisi—sisi sote tulishangaa ni kwa nini Yeye alibaki peke yake? Na kuingia mjini, nanyi mnajua jinsi walivyotutendea.

¹²¹ “Tulipokuwa tukirudi, mnakumbuka tulipokuwa tukipanda vichakani huko nyuma? Tulimsikia akizungumza, na kulikuwako na mwanamke aliyebandikwa mwenye sifa mbaya, naye alikuwa akizungumza Naye. Ni jambo lisilo la kawaida sana kwa mwanamume mwenye heshima kuzungumza na mwa—mwanamke wa aina hiyo. Nasi tukaingia kisiri nyuma ya vichaka tupate kujua kile Yeye angemwambia. Nami ninaweza tu kumsikia Yeye. . . Yale sisi sote tuliyosema, ‘Hebu mwangalieni akimkemea. Hakika atamwambia mahali alipo. Atamwambia kwa sababu yeye ni, yeye ni mwanamke wa aina hiyo. Ninawazia Yeye kweli atamkemea vikali.’

¹²² “Nanyi mnakumbuka jinsi sisi sote tulivyokuwa tukijiandaa kumsikia akimkemea, wakati alipomwambia, ‘Nipe maji ninywe.’ Vema, tulifikiri hilo ni la kushangaza, kwamba Bwana wetu angejhusisha na mtu kama huyo, wa hali duni, Bwana wetu. Mnakumbuka jinsi sisi sote tulivyoangaliana kwa mshangao? Kwa hiyo tulichuchumaa tu nyuma ya vichaka tuone kile Yeye angesema.

¹²³ “Na wakati mazungumzo yakiendelea, basi baada ya kitambo kidogo wakazungumza juu ya dini, na kwa hiyo Yeye akamwambia, ‘Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa,’ naye akasema, ‘Sina mume.’

¹²⁴ “Nanyi mnakumbuka kile sisi sote tulichowazia? ‘Huo ndio wakati mmoja tulipomwona Bwana wetu amenaswa katika mtego.’ Alikuwa amekosea. ‘Sina mume.’ Nanyi mnakumbuka jinsi tulivyopigwa na bumbuazi, ndugu, sisi sote? Bwana wetu amemwambia ya kwamba alikuwa na mume, naye huyu

hapa anakanusha jambo hilo kabisa, 'Sina mume yeyote.' Nasi tukatazamana kwa mshangao. Jinsi ambavyo hatukuweza kutulia kwa dakika moja!" Hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi, haliwezi kutulia hata dakika moja. Mnaona?

¹²⁵ "Kwa hiyo basi tunamwona Bwana wetu, aliposimama kwa unyenyekevu huku ameinamisha kichwa Chake, na kumtazama, kisha kasema, 'Mwanamke, umesema kweli. Wewe ni mkweli, umeniambia kweli.' Ndipo tukashangaa, 'Hapa sasa, Yeye analikwepa kwa kupitia njia nyingine. Yeye alisema, kwanza alisema, "Una mume," naye mwanamke akasema, "Sina mume," na sasa Yeye anakubali ya kwamba mwanamke amesema kweli.' Ndipo mnakumbuka jinsi tulivyojisikia, ndugu?"

¹²⁶ Nao wote wakasema, "Naam, tunakumbuka. Tulia, usiiyumbishe mashua, unaona. Tuko huku mbali kabisa sasa." Na kwa hiyo wote wakasisimkwa, "Naam, ninakumbuka hilo," wote wakizungumza.

¹²⁷ Kisha kasema, "Mnakumbuka, basi, maneno yaliyofuata? 'Umesema kweli. Kwa maana umekuwa na waume watano; na yule unayeishi naye sasa siye wako.'"

¹²⁸ Ndipo tukaangalia *jibu* la mwanamke huyo. Ndipo uso wake ukashuka, macho yake yakametameta, Kitu fulani ndani yake kikashika Moto, ndipo kasema, 'Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii.' Sasa, tulishangaa jinsi Msamaria mwenye sifa mbaya, mwanamke aliyetupwa nje angekuwa na maarifa ya kujua ya kwamba Mtu huyu alikuwa ni nabii.

"Naye alipokuwa akiendelea kuzungumza, mwanamke akasema, 'Tunajua ya kwamba Masihi, atakapokuja, Yeye atatwambia mambo haya. Lakini u Nani Wewe?"

"Naye akasema, 'Mimi ninayesema nawe Ndiye.' Nasi tunaona ya kwamba yeye. . .

¹²⁹ "Tusingeweza kutulia tena, tulifurahi sana kuona kwamba Bwana wetu alikuwa mkweli, nao unabii Wake ulikuwa wa kweli, mpaka tukashangilia kwa furaha, na kukimbia mbele Zake. Ndipo akauacha mtungi wa maji akakimbilia mjini, nanyi mnakumbuka, watu wote wa mjini walikuja huko nje."

¹³⁰ Sasa, kwa kweli mwanamke huyo hakuruhusiwa kufanya hivyo. La. Yeye. . . Kama unajua mwelekeo wa mashariki, na hizo mila, hakuna mtu angemsikiliza, alikuwa mwanamke mwenye sifa mbaya, hakuna mtu angemjali. Hata asingeweza kwenda huko nje, hiyo ndiyo sababu alikuwa huko nje saa tano, asingeweza kutoka pamoja na wanawake waadilifu. Hapa wote wako pamoja, lakini huko asingeweza kufanya hivyo. Na kwa hiyo, kuna. . .

¹³¹ Lakini alipokuwa amekutana na Yesu, naye akanywa maji kutoka kwenye kile Kisima, mtu fulani atamsikiliza, iwe ni halali ama si halali. Hivyo ndivyo ilivyo sasa, mtu anayepata

kunywa kutoka kwenye Kisima hicho, mtu fulani atasikiliza, ni hayo tu. Kama kanisa linakwambia uketi chini au la, jambo fulani litatukia.

¹³² Nafikiri ndugu zangu katika madhehebu yetu yote mbalimbali. . . Hakika na—nakubaliana na Hudson Taylor, yule mmishenari mashuhuri wa India, wakati mvulana mdogo wa Kichina alipookoka, naye akaja, akasema, “Bw. Taylor, itanibidi kuchukua miaka minne ya—ya saikolojia, na kadhalika, na miaka *kadhaa* chuoni.”

¹³³ Bw. Taylor akasema, “Usiache mshumaa uangaze wakati umechomeka nusu, toa nuru yake mara ukiwashwa tu.” Hiyo ni kweli. Shida yake ni kwamba leo, wakati mvulana anapopata wito wa Mungu moyoni mwake, akajazwa na Roho Mtakatifu, anaenda kwenye baadhi ya makaburi haya, ama, seminari, ama ninii. . . Samahani. Kwa vyovyote vile, anaingia mle kwenye hiyo friji, nao wanachukua kutoka kwake kila kitu ambacho Mungu aliweka ndani yake. Hiyo ni kweli.

¹³⁴ Ninaamini saa imewadia. . . Sikubaliani na shule hizi kubwa za theolojia za kujenga siku hizi. Tunazungumza juu ya Kuja kwa Bwana kumekaribia kabisa, na kujenga shule kubwa kubwa na kadhalika. Mbona, matendo yetu wenyewe hunena kwa sauti kubwa kuliko maneno yetu! Tungewezaje kuwa tunaweka nyingi hivi katika majengo, na kadhalika, na shule kubwa kubwa, na kadhalika, huku tukisema Bwana yuaja?

¹³⁵ Ninasema hivi: Mara Mungu anapouwasha mshumaa, shika njia. Kama hujui cha zaidi, waambie tu jinsi ulivyowashwa. Hivyo tu. Acha wao wawashwe, nao watamwambia mtu mwingine, nasi tutakuwa na wakati wa kuwasha mishumaa. Hilo ndilo tunalohitaji kwa vyovyote vile, badala ya theolojia chungu nzima, kuwasha mishumaa. Simulia tu jinsi ulivyowashwa. Ninii tu. . . Hayo tu ndiyo unayopaswa kusema, usijaribu kulihubiri, sema tu jinsi ulivyowashwa, “Nilijazwa na Kitu ambacho kina—kinanichoma moto.” Hivyo tu.

¹³⁶ Simulia tu kuhusu wakati wa kuwashwa, jinsi ulivyowashwa, nao utatoa Nuru unapoendelea kuungua. Acha huyo awashwe, halafu mwingine, ndipo yeye asimulie jinsi ulivyowashwa, naye asimulie jinsi ulivyowashwa, kutakuwako na Nuru hapa baada ya kitambo kidogo kama tu tukisimulia kiasi hicho.

¹³⁷ Sasa, jinsi ambavyo mwanamke huyu, asingeweza kutulia! Akakimbia mjini, nao ushuhuda wake ulikuwa wa kuisimua sana hata wasingeweza kumpuza, kwa hiyo wakatoka nje. Nayo Biblia ilisema ya kwamba watu wa Sikari walimwamini Yesu (Sasa, Yeye hakuwafanyia hivyo tena.), kwa sababu ya ushuhuda wa yule mwanamke ambaye, alimwambia yale aliyokuwa amefanya.

¹³⁸ “Mnakumbuka hapo, ndugu? Sote tulishangaa,” akasema Andrea. “Sote tulishangaa jinsi ambavyo hao Wasamaria kule juu... Sehemu ile ya ardhi ambayo—ambayo Yakobo alikuwa amempa mwanawe Yusufu, naye alikuwa na kisima pale, na sehemu hiyo ya ardhi iliyokuwa imetolewa... Na hapa mwanamke huyu wa Samaria, kitu kichafu kwetu, na hata hivyo, alitambua hilo katika dakika moja, hata katika sifa zake mbaya.

¹³⁹ “Hapana shaka ila katika nyumba yake ndogo ya ukahaba,” ambalo ninakusudia kuhubiri juu yake a—asubuhi, Bwana akipenda, “mahali hapo padogo, alikuwa na magombo fulani ya Mungu pale, ambapo alikuwa akisoma habari za Mungu, na kujua ya kwamba Yeye alikuwa aonekane katika umbo hilo. Na jinsi sisi sote tulivyoshtuka!”

¹⁴⁰ Na loo, ninawazia mtumbwi ulianza kuyumbayumba tena, mtu fulani akipaza sauti na kumsifu Mungu, na huenda ilikuwa ni Petro aliyesema, “Ndugu, hapa pana kina cha futi mia moja na ishirini. Nyamazeni.”

¹⁴¹ Mathayo akasema, “Vema, mnafikiri kwamba mimi... mtapita bila ya mimi kusema kitu?” Mnaona? Kisha kasema, “Hebu niwaambie jambo fulani. Mnakumbuka asubuhi ile ambapo sisi sote tulimtangulia kuuandaa ule mkutano kule Yeriko?”

“Loo, naam,” kasema Luka, “nakumbuka hilo vizuri.”

¹⁴² “Nasi tukamwona maskini mfanyabiashara mmoja kule chini jina la—lake Zakayo, jamaa mdogo, mfupi. Mnakumbuka jinsi alivyokuwa jeuri, jinsi alivyokuwa na kiburi? Maskini Myahudi mwenye pua iliyopinda, na katili jinsi alivyoweza kuwa! Nasi tukamwambia kuhusu Masihi, ‘Loo, nalipata!’

¹⁴³ “Mnamkumbuka mke wake, Rebeka, ambaye alikuwa ni mwaminio wa kweli, jinsi Yesu wa Nazareti alivyomtendea jambo kubwa? Naye akasema, ‘Ninamwombea Zakayo.’ Nasi tuliwazia kama tukienda kwenye mkahawa aliokuwa nao na kula, asingetulipisha. Alipogundua kwamba sisi tulikuwa wanafunzi akatufanya tulipe maradufu, kisha akasema, ‘Tokeni hapa na upuuzi kama huo. Mimi ni rafiki wa Rabbi Kabinski, ama, Labinski, ama...’ Natumaini hakuna mtu kama huyo hapa ndani. Kwa hiyo kwa vyovyote vile, kama nilifanya hivyo, samahani, mnaona.

¹⁴⁴ Kisha kasema, “Kesho yake asubuhi (Rebeka aliomba usiku kucha kwamba...), Yesu alikuwa anaenda kuutembelea mji huo, na kwa hiyo akawazia ya kwamba alitaka akutane na Yesu. Alikuwa amemwambia kuhusu Yeye kuwa ni Nabii, Naye alikuwa ni Nabii ambaye Musa alinena habari zake. Lakini, loo, alikuwa na kiburi! Matumaini yake yalikuwa kwenye pesa, wala hakujali chochote kuhusu Yesu wa Nazareti. Lakini mnajua, wakati Rebeka alipotwambia aliomba usiku kucha... Mwajua, maombi hubadilisha mambo.”

¹⁴⁵ Hiyo ni kweli, marafiki. Mnajua, maombi hubadilisha nia ya Mungu. Mungu alimtuma nabii kwa mtu fulani siku moja na kusema, “Tengeneza mambo ya nyumba yako; utakufa.” Akaelekeza uso wake ukutani, na kuomba kwa bidii, na kusema, “Bwana, ninakusihi unifikirie, nimetembea mbele Zako kwa moyo mkamilifu. Ninahitaji miaka kumi na mitano.” Na ilionekana kana kwamba Mungu angalizungumza moja kwa moja tena na mfalme, alikuwa ndiye mtu mkubwa kuliko wote nchini, bali Yeye hunena na nabii Wake. Alimwambia tu Isaya, “Rudi ukamwambie, nilimsikia nami nitayaokoa maisha yake.”

Ungeweza kuwazia aibu ya nabii huyo, kwenda mara moja kwa askari, “Loo, nabii mkuu, vipi kuhusu mfalme wetu?”

“BWANA ASEMA HIVI, atakufa.”

Kaenda kwa watu maskini waliosimama langoni, “Vipi kuhusu nabii wetu. . . ? Nabii, vipi kuhusu mfalme wetu?”

“BWANA ASEMA HIVI, atakufa.”

¹⁴⁶ Loo, jinsi walivyokuwa wakilia! Akija moja kwa moja, akitangaza, “BWANA ASEMA HIVI, atakufa.” Halafu basi, katika dakika chache, huyu hapa anarudi akisema, “BWANA ASEMA HIVI, ataishi. BWANA ASEMA HIVI. . .” Ilikuwa je? Maombi yalibadilisha mambo. Maombi hubadilisha mambo.

¹⁴⁷ Angalieni, halafu ushuhuda huu, “Maskini Zakayo asubuhi hiyo, wakati Rebeka alipokuwa ameomba usiku kucha, kesho yake asubuhi anaamka mapema sana, naye anaanza kujiandaa, na kuchanua ndevu zake, na kuvaa joho lake lililo bora zaidi, mwajua, na kujiweka tayari kushuka kwenda mjini, naye Rebeka akageuka, mwajua, na kwa namna fulani kuchungulia kwa jicho moja, na kusema, ‘Uh-huh. Kumbé, asante, Bwana. Itakuwa sawa. Unaenda wapi asubuhi ya leo, mume wangu mpendwa?’

¹⁴⁸ “‘Loo, natoka tu nje kupumua hewa.’ Naye anashuka kwenda langoni, ndipo anakuta kwamba hawezi kufika kule, kuna wengi sana kule, yeye ni mfupi sana wa kimo. Anarudi chini na kuchukua ndoo ya takataka ya mji, na kuisukumia kwenye mti, anapanda juu ya mti, kasema, ‘Ninajua Yeye anashuka kwenye Barabara ya Utukufu hapa, na kugeukia Barabara ya Haleluya.’” Yeye hufanya hivyo daima. “‘Kwa hiyo nitakutana Naye papa hapa kwenye kona.’” Hapo ni mahali pazuri pa kukutana Naye.

“Kwa hiyo mnakumbuka, ndugu, jinsi Zakayo alivyotwambia habari zake?”

“Naam, tunakumbuka jambo hilo.”

¹⁴⁹ “Ndipo akapanda juu ya mti huu, naye akasema, ‘Sasa, mimi ni mdogo sana hivi kwamba wakati Yeye anapopitia hapa, akipita hapa, Yeye kamwe hataninii. . . Kamwe sitamwona, wala Yeye kamwe hataniona, lakini nikipanda juu ya mti huu,

niko juu ya umati wote, ninaweza kuangalia moja kwa moja chini na kumwona, na karibu nitamwambia ukweli wa mambo atakapopitia hapa chini.’

¹⁵⁰ “Ndipo basi muda si muda mwajua, mbona, ilitokea tu aliwazia, ‘Mnajua nini? Rebeka alisema ya kwamba Mtu huyo alikuwa ni Nabii. Na kama Yeye alikuwa ni Nabii, huenda akaangalia juu kwenye mti huu na kuniona, nami ningeaiibika, kwa hiyo nitamhepa, Yeye hataniona.’ Kwa hiyo akaanza kujizungushia majani, naye akajificha vizuri sana. Akaketi kwenye panda la mti pale apate kujipangusa vibanzi, na takataka kutoka kwenye ile ndoo, mwajua, na kadhalika.”

¹⁵¹ Lakini utafanya mambo ya dhahaka wakati u—unapotaka kumwona Yesu, hakuna kitu kitakachokuzuia. Wanaweza kuwaita watakatifu wanaojibingirisha ama chochote unachotaka. Wewe, kama umeamua kumwona Yesu, utaenda kumwona kwa vyovyote vile.

¹⁵² “Kwa hiyo huyo hapo ameketi mahali ambapo matawi mawili...” Sasa, hapo ni mahali pazuri ambapo kila mtu hufikia, ambapo njia yako na njia ya Mungu hukutana. “Naye akaketi kwenye tawi hili, akavuta matawi na kujifunika kabisa, akasema, ‘Kamwe hataniona.’ Kwa hiyo akajifanyia mlango, jani kubwa hapa, ili aweze kulivuta jani hili juu, na kuangalia, naye angeweza kumwona Yeye akiya, kisha alirudishe. Akaangalia kila mahali, hakuna njia Kwake kumwona. Baada ya kitambo kidogo akasikia kelele.”

¹⁵³ Mnajua jambo la kigeni? Yesu akiwa karibu, kuna kelele nyingi sana. “Kwa hiyo akamwona akiya, akainua jani hili, naye akamtazama, lakini Yeye, kulikuwa na kitu fulani kumhusu kilichoonekana tofauti, hakuwa kama watu wengine. Tunamwona yule mvuvi mkubwa akienda zake akisema, ‘Simile, ndugu. Samahani, siwezi...hatuwezi kuwaruhusu karibu na Yeye. Amechoka, amekuwa akihubiri karibu usiku kucha. Samahani, jamani, hatuwezi...’

¹⁵⁴ “Na alipokuwa akipita, (Mnakumbuka yale Zakayo aliyosema?) alikuwa ameinamisha kichwa chake, akaja moja kwa moja na kusimama chini ya huo mti, ndipo aliposimama chini ya huo mti, aliangalia juu, na akasema, ‘Zakayo, shuka chini; ninaenda nyumbani pamoja nawe kwa chakula cha kutwa.’

“Loo, mnakumbuka yale Zakayo aliyosema? ‘Hilo lilitosha. Alijuaje kwamba mimi ni nani? Naye alijuaje nilikuwa mtini?’”

Zakayo, hapa usiku wa leo, Yeye anajua hasa mahali ulipo, na kwamba unajificha kwenye majani gani. Kweli kabisa.

¹⁵⁵ Mmoja wao huenda alisema, “Ninii tu...” Sasa, hebu na tuache Marko ashuhudie mara moja, na ndipo tutafunga. Huenda Marko alisema, “Sikilizeni, mnakumbuka Bartimayo, yale aliyosema? Alikuwa ameketi pale asubuhi nzima, kila kitu,

matumaini yote yalikuwa yamekwisha, naye akasikia kelele ikitoka mjini. Basi ilitokea kwamba alikumbuka, alipokuwa ameketi pale akisoma, na kuwazia, ‘Unajua nini? Kama ningaliishi katika siku za manabii, moja kwa moja kwenye barabara hii walikuja Eliya na Elisha, wameshikana mikono, wakishuka kwenda kuvuka Yordani, kama ningaliishi katika siku hizo, ningalikimbia kule mbele ya hao manabii, na kuanguka chini, na kusema, “Loo, watu mashuhuri wa Mungu, niombeeni nipate kuona!” Lakini ole, kuhani ananiambia ya kwamba siku za miujiza zimepita.’

¹⁵⁶ “Basi wazia tu, yadi mia moja kutoka mahali ninapoketi, yule shujaa mkuu, Yoshua, alikuwa akitembea alasiri moja, na mara akamwona Mtu amesimama karibu naye akiwa na upanga uliochomolewa, Yoshua akauchomoa upanga wake, akamwendea mbio, naye akasema, “Je, Wewe uko upande wetu? Je, uko upande wa adui yetu?”

¹⁵⁷ “Naye akainua upanga, nayo radi ya zigizaga ikaruka kutoka kwake, na kusema, “Mimi ni Kapteni wa jeshi la Bwana.” Naye Yoshua, yule shujaa mkuu, akatupa chapeo yake chini, akaweka upanga wake chini, akaanguka miguuni Pake. Wazieni tu, hiyo ilikuwa tu yapata yadi mia moja na hamsini, ama mia mbili kutoka mahali ninapoketi.’

¹⁵⁸ “Hakujua ya kwamba Kapteni Mkuu yule yule alikuwa njiani akipitia kule wakati huo.” Watu hawajui ya kwamba Kapteni Mkuu yuyo huyo, yuko moja kwa moja katika jengo hili, usiku wa leo. La sivyoyote, Biblia ni Kitabu cha kupotosha, Yeye alisema, “Walipo wawili watatu wamekusanyika nitakuwa kwa jina lao . . . nitakuwa katikati yao, ambapo wamekusanyika katika Jina Langu.”

¹⁵⁹ “Akasikia kelele.” Sasa, Marko anawapa ushuhuda wa yale ambayo huenda alimwambia. “Ndipo mara kukaja, kelele nyingi sana, ndipo mtu fulani akasema, ‘Ni nani anayepita hapa?’ Na baadhi yao wakasema *jambo moja* na *lingine*, na muda si muda mwajua, tukamsikia kasisi mmoja akilia, na kusema, ‘Aisee, tunasikia ya kwamba unawafufua wafu. Tuna uwanja mzima wa makaburi uliojaa hao hapa juu, panda hapa ukamfufue mmoja wa hawa.’”

¹⁶⁰ Mwajua, maskini ibilisi huyo hajafa bado. La, bwana, “Ikiwa wewe!” Yuyo huyo akaweka kitambaa usoni Mwake, na kumpiga kichwani kwa fimbo, na kusema, “Kama wewe ni nabii, tuambie ni nani aliyekupiga, tutakuamini.” Mnaona? Ibilisi yuyo huyo wa kale aliyesema, “Kama wewe ni Mwana wa Mungu, tuna mtu fulani hapa chini, fanya mwujiza *huu*. Hebu tukuone ukiufanya.” Mungu hamfanyii vitimbi mtu yeyote.

Yesu alisema, “Nimekuja kufanya mapenzi Yake, wala sifanyi neno mpaka Yeye aniambie kwanza,” Yohana Mtakatifu 5:19.

¹⁶¹ “Kwa hiyo maskini Bartimayo kipofu akarudishwa nyuma. Tuliwasikia wote, mmoja kwa ajili Yake, mmoja akisema, ‘Hosana kwa Nabii ajaye katika Jina la Bwana!’ Na mwingine akisema, ‘Mwondoeni mnafiki kama huyo! Umati uliochanganyika namna hii!’” Daima kuna umati uliochanganyika mahali Yeye alipo.

¹⁶² Nasi tunaona ya kwamba maskini Bartimayo kipofu, kama uliwahi kwenda Yeriko na kuona mahali alipoketi, kufikia mahali Yesu alipokuwa, ilikuwa karibu yadi mia mbili.

¹⁶³ Hapo umati huo, ukimtupia matunda yaliyoza, na kadhalika, na kumdhihaki, bali uso Wake wa thamani ulikuwa umelekezwa Kalvari, Yeye alikuwa akipanda kwenda kuwa Dhabihu kwa ajili ya ulimwengu. Mzigo wote wa dhambi uliwekwa juu Yake, Mungu alikuwa ameweka juu Yake uovu wetu sisi sote. Alikuwa akitembea, bila kujali yale waliyosema, Yeye angefanya yale Baba aliyomwambia afanye, na hilo lilitosha.

¹⁶⁴ “Naye alikuwa a—akitoka Yeriko, akitoka nje ya mji, na muda si muda mwajua, Bartimayo kipofu akasema, ‘Ni nani? Ni nani Huyu? Kelele hizo zote ni za nini?’

“Ndipo mtu mmoja akamsukuma nyuma, ‘Loo, nyamaza, wewe ni mtu asiye na maana,’ akamsukuma nyuma, matambara yake yaliyochakaa, akainuka kutoka mavumbini.

¹⁶⁵ “Hapana shaka kulikuwako na mwanamke Mkristo mzuri, ambaye alikuwa mwaminio wa Bwana Yesu, kamwe wasingeweza kuvumilia kumwona kipofu akisukumwa huku na huku, daima wana huruma, watumishi wa Yesu, kwa hiyo huenda msichana huyu aliinama chini na kusema, ‘Bwana, naweza kukusaidia?’

“Na, ‘Naam, Mama. Nataka uniambie, hizo kelele zote ni za nini?’

“‘Loo, kwani wewe ni mgeni hapa?’

“‘La, nililelewa hapa.’

“‘Vema, Huyu ni Yesu wa Nazareti, yule Nabii wa Galilaya.’

“‘Sielewi.’

“‘Je, unayafahamu Maandiko?’

“‘Naam.’

“‘Unamjua yule Yesu wa Nazareti, yule Nabii ambaye Musa alisema atainuliwa? Yeye anapita, Huyu ni Yeye.’”

¹⁶⁶ “Ndipo kwa ghafla Bartimayo, akang’amua, ‘Yuko mbali sana kwangu kumruhusu anisikie kimwili, kwa sababu kuna watu wengi sana. Lakini kama Yeye ni Mungu, kama huyo ni Mwana wa Daudi, bado ninaweza kumgusa.’ Huenda alipiga magoti na kusema, ‘Ee Mungu, unisikie, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu!’ Asingelisikia ninii yake, kwa masikio Yake hasa,

lakini imani ya ombaomba huyo mmoja kipofu ilimsimamisha Yesu.”

Ningependa kuhubiri siku moja, ama wakati fulani kabla sijaondoka: *Ndipo Yesu Akasimama Kimya*. Naam.

“Naye akasimama kimya, wala hakujua. Ilikuwa ni kitu gani? Imani Yake ilimsimamisha, ndipo basi akamleta.”

¹⁶⁷ Loo, ni mkutano wa jinsi gani wa ushuhuda! Wakaanza kuangalia huku na huku, ilikuwa inachelewa. Kasema, “Ndugu, afadhali tuingie ufukoni.” Kwa hiyo wakaanza kuvuta tena.

¹⁶⁸ Mnajua nini? Ibilisi akawaona huko nje bila Yeye, naye akaangalia juu ya kilele cha kilima, akasema, “Hao hapo wameondoka bila yeye, na sasa ni nafasi yangu.”

¹⁶⁹ Sasa, nasema hili kwa upendo, ndugu. Mnaona? Nashangaa kama hivyo sivyo hali ilivyo usiku wa leo. Tangu uamsho umekuwapo, ule ufanisi mkuu wa kanisa, tumejenga majengo mapya, tumekuwa katika mipango mikubwa, tumefanya kila kitu kikubwa ambacho kingeweza kufanywa; na kujaribu kujilinganisha na Walutheri, Methodisti, na Katoliki, tukiingiza wafuasi wengi zaidi wakati wote. Sijui kama, mpango wetu mkubwa, kama hatujaondoka bila Yeye katika msisimko wetu.

¹⁷⁰ Walikuwa wamesisimkwa sana, hawakumlazimisha, waliondoka bila Yeye. Na hiyo ilikuwa ndiyo nafasi ya ibilisi ku—kuanza nao wakati huo. Kwa hiyo akashuka na jeshi lake lote, akasema, “Nimewapata sasa bila yeye, kwa hiyo nitawazamisha huko nje kwenye hiyo bahari.” Ndipo akaanza kupuliza pumzi yake kutoka angani.

¹⁷¹ Naye ameanza kuipuliza tena, “Siku za miujiza zimepita. Yote ni mhemko. Yote ni ulokole. Yote nii *haya, yale*, ama *mengineyo*.”

¹⁷² Nazo hizo mashua ndogo zinayumbayumba sana, mwajua, bila tanga. Mashua ikajaa maji, makasia yakavunjika, mlingoti wa hema ukavunjika vipande viwili, nao upepo ulikuwa umeipigapiga, na kuirusharusha huku na huku. Ilionekana kana kwamba matumaini yote yalikuwa yamekwisha kwamba wangeokolewa.

¹⁷³ Lakini unajua nini? Alipowatuma, mnajua alilofanya? Alipanda mlima ulio mrefu sana uliokuwepo huko nje. Kadiri unavyozidi kwenda juu, ndivyo unavyoweza kuona mbali zaidi. Kwa hiyo akapanda mlimani kusudi aweze kuwaangalia.

¹⁷⁴ Na wakati alipokufa pale Kalvari, na akawaagiza wanafunzi Wake kwenda ulimwenguni kote: “Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio,” Alipanda kutoka Kalvari akalipita jua, mwezi, na nyota, moja kwa moja kupita Njia ya Kilimia Cheupe. Alienda mpaka akapita Mbingu. Biblia ilisema Yeye ameketi hata juu ya Mbingu, antazama chini Mbinguni. Alifika kule

kusudi aweze kuona kote ulimwenguni. “Na jicho Lake liko juu ya shorewanda,” nami ninajua Yeye anaangalia usiku wa leo.

¹⁷⁵ Haidhuru inaonekana tumerushwa-rushwa jinsi gani, ni makasia mangapi yamevunjika, matumaini yote yamekwisha kiasi gani, Yeye angali anaangalia, “Sitakuacha wala sitakupungukia.”

¹⁷⁶ Loo, katika wakati huo wa hatari uamsho ulikuwa umekwisha, nayo mashua ilikuwa imejaa maji, na ilionekana kana kwamba kila kitu kilikuwa kimekwisha, matumaini yote yalikuwa yamekwisha, naye Huyu hapa anakuja, akiwaendea juu ya bahari, akitembea juu ya bahari. Ajabu, kutembea juu ya bahari, na sehemu ya ajabu ni, Kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia, walikiogopa. Kilionekana ni mzuka, kilionekana kama roho fulani, nao wakalia kwa hofu.

¹⁷⁷ Hilo ni jambo lile lile leo hii. Kitu pekee kinachoweza kutuokoa ni Biblia, na ahadi ya Mungu, na Roho Mtakatifu pamoja nasi. Inaonekana ya kutisha kwa watu, nao wanalia kwa hofu. Lakini hii hapa inakuja ile Sauti ndogo tamu, tulivu: “MsioCOPE; Ni Mimi.”

¹⁷⁸ Nami ninaamini, usiku wa leo, kama angeweza kuja kwenye mkutano huu usiku wa leo, akifanya miujiza Yake, nanyi mkishangaa ni kitu gani kinachotukia, “Ni kitu gani kinachofanya hivyo? Ni ujanja wa aina gani? Je, ni ninii—ninii . . . telepathia fulani? Ni kitu gani?” Angekujibu kwa sauti kuu, “UsioCOPE; jipe moyo; Ni mimi,” akitimiza ahadi aliyosema angefanya.

Lakini Kitu chenyewe ambacho kingeweza kuwasaidia, na Kitu pekee kingeweza kuwasaidia, walikiogopa.

¹⁷⁹ Na siku hizi, ni jambo lile lile, wanaogopa kumshika Roho Mtakatifu, wanaogopa kuamini Ujumbe wa Mungu, wanaogopa kumwamini Roho Mtakatifu wanapomwona akitenda kazi miongoni mwao. Watasema, “Sasa, ngoja kidogo, sijui kama inaweza kuwa ni kwa ajili yangu au la.” Ni kwa “yeyote atakaye,” uponyaji ni kwa kila mtu, wokovu ni kwa “yeyote atakayekuja,” mtu yeyote.

¹⁸⁰ “MsioCOPE; Ni Mimi.” Ni Kristo, Yeye hajafa, Yeye yu hai milele, na anazo funguo za mauti na kuzimu. Wala hakuna kitu kinachoweza kudhuru. Unaamini hilo? Mungu anabaki Mungu. Kama aliwahi kuwa Mungu, Yeye angali ni Mungu. Mnaamini hilo? Amina.

¹⁸¹ Nimewachelewesha kila usiku, sitafanya hivyo sasa. Ni wangapi hapa ndani wasio na kadi ya maombi, ambao hawanijui mimi, ama siwajui ninyi, nawe uko tayari kusema kwamba “Ninaamini ujumbe huo, ukweli kwamba Yesu Kristo yuko katikati yetu”? Inueni mikono yenu, popote mlipo. Sasa, Mungu wa Mbinguni na aje akitembea juu ya bahari iliyochafuka,

wakati unaposhangaa, “Nitapataje kadi ya maombi? Nitapataje kuumbewa?”

¹⁸² Si... Huenda... Huenda nikawaombea, niwawekee mikono, huenda ndugu wakaomba, sisi ni wanadamu, huyo siye Mtu wa kungusa hata hivyo, sisi ni watu wanaowahurumia, bali Yule wa kungusa ni *Yeye*, huyo Ndiye, mguse *Yeye*. Na kama mtu mwingine anaweza kungusa, hakika unaweza, kwa kuwa *Yeye* anagusika.

¹⁸³ Biblia ilisema ya kwamba *Yeye* ni yule yule jana, leo, na hata milele. Biblia ilisema *Yeye* ni Kuhani Mkuu, sasa hivi, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Vema, kama *Yeye* ni Kuhani Mkuu yeye yule, angetenda vile vile kama alivyotenda wakati mtu fulani alipomgusa katika siku hiyo kwa imani. Ni wangapi, siku hiyo pamoja na yule mwanamke aliyetokwa na damu, ni wangapi waliokuwa wakimgusa, wakimkumbatia wakisema, “Rabi, tuna furaha kukuona Wewe, Bwana,” kadhalika namna hiyo, Naye akasimama na kusema, “Mtu fulani amenigusa”?

¹⁸⁴ Ndipo Petro akamkemea, kama kusema, “Bwana, unajua hilo ni kudhalilisha ninii Yako—hadhi Yako? Wewe kuuliza ni nani aliyekugusa, wakati kila mtu ameweka mikono yake juu Yako, akikugusa.”

¹⁸⁵ Akasema, “Naam, lakini huu ni mguso wa aina nyingine.” Mnaona? “Nimekuwa dhaifu, nguvu zimenitoka.” Ndipo akaangalia kote kwenye kusanyiko, na akamwona maskini mwanamke huyo. Loo! Naye alimwambia nini kuhusu kutokwa kwake na damu? “Imani yako imekuokoa.” Kama huyo alikuwa ni Yesu jana, huyo ni Yesu leo. Basi ndugu, dada, hebu niwaulizeni jambo fulani.

¹⁸⁶ Sasa, hutamwona Yesu katika mwili wa kawaida mpaka atakapokuja kwa ajili ya Kanisa Lake. Lakini kila kitu alichokuwa, yote—yote aliyokuwa Mungu aliyamimina ndani ya Yesu, na yote aliyokuwa Yesu aliyamimina ndani ya Kanisa. Ni yeye yule, *Yeye* yuko ndani ya Kanisa, waaminio. Sasa, kama—kama mtu akija hapa, kama nilivyosema hivi majuzi usiku, akiwa na makovu ya misumari na—na alama za miiba kichwani mwake, huyo angeweza kuwa mdanganyifu. Lakini unapoona Maisha yenyewe ya Kristo yakitolewa! Marko... Yohana 14:12, *Yeye* alisema, “*Yeye* aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya; nyingi kuliko hizi atafanya; kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu.”

¹⁸⁷ Lakini inaonekana kwamba baadhi ya watu wanafikiri hivyo, kwamba watu wanaobeba karama hizi za wahudumu wanapaswa kuwa kasisi fulani mashuhuri, msomi fulani mashuhuri. Nina wangu wa kwanza niliyepata kusoma katika historia, ambaye Mungu aliwahi kumtumia namna hiyo. Niambieni mahali alipo, na wakati lilipotukia. Mungu sikuzote

huchukua kitu duni, ili kwamba aweze kuonyesha utukufu Wake kwa kitu duni.

¹⁸⁸ Angalia wale aliowachagua: wavuvi, wasio na elimu, wasio na maarifa, apate kujidhihirisha Mwenyewe. Huenda ukaniambia kuhusu Paulo. Paulo alisema ilimbidi kusahau kila kitu alichowahi kujua apate kumjua Kristo, alikufa kila siku apate kumjua Kristo. Naye akasema, “Mimi kamwe,” akawaambia Wakorintho, “Sikuja kwenu na maneno makuu ya elimu, na werevu, kama watu wenye elimu, kwa sababu imani yenu ingejengwa katika hayo. Lakini nilikuja kwenu katika nguvu za Roho, ili imani yenu iwe katika—katika Kristo, katika Roho.”

¹⁸⁹ Mungu huwachukua watu kutoka kwa mtu yeyote anayetaka kumchukua, duni, apate kujidhihirisha Mwenyewe. Hilo ndilo linalomfanya Yeye Mungu, si mtu huyo basi, ni Mungu akifanya kazi katika kitu duni, akithibitisha ya kwamba ni Mungu. Kama mtu huyo alikuwa kitu fulani, ungeweza kumwanguka mtu huyo, lakini kama mtu huyo si kitu, basi haina budi kuwa ni Mungu. Na katika kisa hiki, hakuna mtu angaliweza kufanya hivyo, haina budi kuwa ni Mungu, na ni kutimiza ahadi Yake. Sasa, tunajua jambo hilo.

¹⁹⁰ Basi rafiki, simama kwa dakika moja tu, tikisa kumbukumbu ya—ya—yako, tikisa se—sehemu ya... pulizia mbali mavumbi kutoka kwa ahadi za Mungu uone kama hatujaahidiwa jambo hili katika siku za mwisho. Sasa Yeye anaonekana miongoni mwa watu Wake, Naye yupo hapa, usiku wa leo. Na haidhuru angenipaka mafuta kiasi gani, hana budi kukutia mafuta vivyo hivyo. Nayo ni imani yako, si yangu, ni imani *yako* inayofanya jambo hilo, si yangu hata kidogo. Mimi ni chombo tu, nawe ni chombo tu, ambacho kama watu fulani...

¹⁹¹ Sasa, kama hili likimgusa mtu aliye na—aliye na kadi ya maombi ambaye ataombewa, silimaanishi hivyo. Lakini nataka kuwaulizeni jambo fulani. Wengi wenu huko nje... Simwoni mtu ila wale niliowatambulisha, sininii... Hata sikuwaona.

¹⁹² Nilimkosa mmoja, Ndugu na Dada Dauch, wanaoketi *hapa*, kote kutoka huko juu Ohio, wakaja huku chini. Laiti ningalikuwa na wakati wa kutoa ushuhuda wao. Jinsi mtu, mwenye umri wa miaka tisini, angeyastahimili mambo hayo, naye hutufuata popote tuendapo! Naam, hiyo ni kweli, kwa sababu anaamini. Na jinsi ambavyo ushuhuda wao ungekushtua! Lakini mbali na Ndugu na Dada Dauch wanaoketi hapo, pia ninaamini Ndugu na Dada Simpson (Sasa, akina Sothman na hao wengine wako *huko* nyuma mahali fulani, bali mimi sijui.), Simjui mtu yeyote, Ndugu Roberson, na hata sijui jina la mwenyekiti ni gani. Hiyo ni kweli, nisingeweza kuwaambia jina lake sasa hivi kama ilinibidi kuwaambia. Sijui, nimelisikia, lakini sijui.

¹⁹³ Na siku nzima...Leo nilimchukua mwanangu mdogo, Joseph, tukaenda ufukoni mwa bahari, nami nikaegesha gari kwenye ghuba ndogo, kisha nikasema, "Joseph, cheza huko nje, sina budi kupanda hapa juu kwenye ghuba ndogo." Na wakati...Nikasema, "Mungu, Wewe mshughulikie mwanangu hapo, asiye akaingia katika mawimbi hayo." Nikapanda kwenda kuzungumza Naye.

¹⁹⁴ Mimi si mtu anayejitenga, lakini huwezi kuwa mtumishi wa Mungu na mtumishi wa umma. Huwezi, huko nje kwenye karamu na kupiga makelele namna hiyo, na bado utarajie kubaki...huna budi kujiweka mwenyewe kwa Mungu, ili uweze kuusaidia umma. Na hilo ndilo lililonileta hapa, ni kuwasaidia, sikuja hapa kwa ajili ya umaarufu. Mbona, mlijua ninajiepusha na upuuzi kama huo! Nami ninajua kwamba mimi si kitu.

¹⁹⁵ Sikuja hapa kwa ajili ya pesa. Mbona, bila shaka sivyo! Sikuja hapa kwa sababu sikuwa na mahali pengine pa kwenda, nilikuja hapa kwa sababu nilijisikia kuongozwa kuja hapa. Nina mialiko mia sita au zaidi kutoka ng'ambo na kadhalika, Wafanyabiashara Wakristo kutoka kila mahali, matawi ya kuanzishwa ulimwenguni kote, nauli imelipwa, kila kitu. Si lazima niwe na pesa, kila mahali niendapo, ninii...wanalipa tu. Wafanyabiashara wakitaka kunituma mahali fulani, wakati mwingine wanatumia dola thelathini, arobaini elfu kwa mwaka kunituma mahali mahali, wala sina haja ya kuwa na senti moja.

¹⁹⁶ Kama nikitaka kuninii...Kama Mungu akinituma ambako kuna watu watano ama sita tu, ninaweza kwenda, nikae mpaka atakaponiambia niondoke. Mnaona? Siwajibiki, ila tu kwa Mungu. Ndipo sina budi kutafuta kujua, "Baba, ninafanya nini hapa? Unataka nini, mimi hapa?"

¹⁹⁷ Yesu alipanda kwenda Sikari, alikuwa akienda Zake Yeriko. Kwa nini? Baba alimtuma tu huko juu. Sasa, ni kitu gani kitakachofuata? Huyu hapa mwanamke anatokea, kwa hiyo Yeye alizungumza tu na huyo mwanamke, akapata kujua ilikuwa ni kitu gani, nao mji wote ukamwamini.

¹⁹⁸ Sasa, Yeye yupo hapa usiku wa leo. Basi liaminini hilo, msitie shaka. Wewe amini moyoni mwako ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, Naye alifufuka katika wafu na kupaa juu, baada ya kuteswa na kusulubiwa na Pontio Pilato, na kuzikwa na kufa kaburini siku tatu, na kufufuka, na kupaa juu, naye ameketi mkono wa kuume wa Ukuu kwa Mungu, usiku wa leo. Yeye ni Kuhani Mkuu aliye hai, anayeishi daima kutuombea tunapokiri, na Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, yeye yule jana, leo, na hata milele, pamoja na kila ahadi na mambo aliyofanya yapate kuonyeshwa tena Kanisani.

¹⁹⁹ Baada ya parare wa Kirumi na tunutu kuula wote, Yeye aliahidi angerudisha, asema Bwana, katika siku za mwisho, Yeye angeurudisha moja kwa moja tena, Mti huo wa Bibi-arusi.

200 Yeye alikuwa ni ule Mti, ule Mti wa Uzima tangu bustani ya Edeni, ambapo, mwanamke alikuwa ni mti wa mauti, upotovu, huo ndio unaowafanya watende jinsi wanavyotenda siku hizi. Kitu hicho chote kimekuwa ni upotovu, wakitenda hivyo.

201 Ni vigumu sana kulipinga, bali huna budi kusimama, mtu fulani hana budi kulisema. Bila shaka. Utakuwa maarufu zaidi kama hukulisema, lakini ni nani atakayelisema? Mtu fulani hana budi kusema jambo fulani kulihusu, maana Mungu... ndipo itakuwa, wanawajibika basi kwenye Siku ya Hukumu. Lakini kama hawakuninii... kama walilisikia na kulipuuza, hilo ni juu yao. Lakini sasa, kulisikia, kutembea ndani yake!

202 Sasa, naomba Roho Mtakatifu, ambaye ninamwakilisha hapa usiku wa leo, miongoni mwa mwili wa Kristo, na aondoe kila hofu na mashaka kutoka kwenu, jalia ashuke aje hapa usiku wa leo, kama tu alivyofanya usiku ule juu ya bahari na kusema, "MsioCOPE, ni Mimi, yeye yule jana, leo, na hata milele."

203 Jinsi bango hilo lilivyofaa! Sikujua lilikuwako mpaka jana usiku; walilichapisha huko juu. Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Sasa, wewe amini kwa moyo wako wote.

204 Ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Kama atafanya hivyo angalau, mara moja inapaswa kutosha, lakini mara mbili, mara moja ama mbili, katika jengo hili usiku wa leo... Nasi hatuko nje... Si kama uchawi fulani chini ya ubao fulani wa ouija mahali fulani, tuko papa hapa chini ya taa za maskani hii, tuko papa hapa chini ya... kila kitu kiko wazi hapa, katika Uwepo wa Mungu, na mbele ya umati huu, pamoja na Biblia ya Mungu *hapa*, ikitangaza litatukia. Hapo ndipo imani yangu inaposimama, papo hapo, ambapo Yeye alisema jambo hilo. Yeye aliahidi jambo hilo, nami ninajua atalitimiza.

205 Yule Malaika, wakati alipokutana nami usiku huo kule juu, na ile Nuru ikizunguka-zunguka kupitia kule, naye akaniambia mambo hayo na kusema, "UsioCOPE. Sasa, itakuja kutimia *hili*, na halafu itakuja kutimia *lile*," wengi wenu mnakumbuka wakati ilipotabiriwa, hii hapa. Sasa, ninawaambia kweli, Kristo yupo hapa, nanyi tayari mmeponywa, kila mmoja wenu, kila mtu ameokoka, bali huna budi kulikubali lipate kukufanyia lolote. Huna budi kuliadini, na kulichukua katika ninii yako mwenyewe... "Ni kwa ajili yangu." Gharama imelipwa, inakubidi tu kuliadini.

206 Sasa, kama Yeye angefanya hivyo, ni wangapi hapa ndani wangesema, "Kwa neema na msaada wa Mungu, nitaukubali usiku wa leo, kwa ajili ya Mwokozi na Mponyaji wangu pia"? Inueni mikono yenu na kusema, "Mungu, ninamaanisha hilo kutoka kwenye kilindi cha moyo wangu, nitafanya hivyo." Mungu awabariki, inaonekana kama asilimia mia moja kila mahali. "Ningeninii... Ninafanya hivyo."

207 Sasa, tuna magumu, mnajua nina hayo, nami ninapiga vita kwa nguvu dhidi yake. Lakini Mungu atatuza hilo, kamwe msiwe na wasiwasi kuhusu hilo, mnaona, imekuwa hivyo daima.

208 Ninakumbuka, hapa si muda mrefu uliopita, jamaa mmoja alikuja, aliyeajiriwa na jeshi, alikuja kunipumbaza akili. Mnakumbuka huo mkutano. Aliketi huko nje, nami nikaendelea kuhisi roho ya kigeni mahali fulani, nikajaribu kuipuuza, kwa sababu mambo mengi sana yamefanywa, maovu. Kamwe sikusema lolote, niliendelea kwa muda kidogo. Aliendelea tu kufanya hivyo. Angeingia—angeingia katika kambi za jeshi, na kuwafanya wavulana wabweke kama mbwa, na kukimbia huku na huku kwenye ninii yao. . .

209 Roho Mtakatifu alinichukua tu, nisingeweza kusema cha zaidi, nikasema, “Ewe mtoto wa ibilisi! Kwa nini umekuja kukatiza mkutano wa Bwana? Mungu atakushughulikia.” Naye amepooza tangu wakati huo, kwa hiyo. . . Alituma barua baada ya barua, na kusema *hili, lile, na linginelo*. Nikasema, “Sina uhusiano wowote nalo, Bwana. Kamwe sikufanya hivyo. Tubu! Ndilo jambo pekee ninaloweza kukwambia. Hiyo ni kati yako na Mungu.”

210 Sasa, ninachukua kila roho hapa ndani chini ya mamlaka ya Roho Mtakatifu, Ambaye ananitia upako sasa, katika Jina la Yesu Kristo. Jalia utukufu wa Mungu uangaze kote, na kuthibitisha, haidhuru nisemacho. . . Ninaweza kusema uongo, mimi ni mwanadamu, bali Mungu hawezi kusema uongo, Yule aliyeahidi jambo hilo.

211 Iweni tu katika maombi, semeni tu, “Bwana Yesu, mtu huyu haniujui, lakini tunaambiwa ya kwamba Wewe utalituma hili. Nimekuwa hapa usiku baada ya usiku, nami nikayachunguza Maandiko, ni kweli kabisa.” Nayo ndiyo ishara ya mwisho ambayo tutapokea kutoka kwa Mungu, mpaka Moto utakaposhuka, kama tu ilivyokuwa katika Sodoma ambapo Yesu aliahidi, na akasema sisi ni. . . hilo ndilo jambo letu la mwisho, ishara ya mwisho. Na huo ndio ukweli. Wewe liandike tu neno langu katika kitabu chako mahali fulani na uone kwamba hiyo ni kweli.

212 Angalia katika mwaka wa '46, yale aliyosema kuhusu kurudi kwa Billy Graham, na hao wengine na kadhalika, ule uamsho, na kile kingetukia. Mbegu za kimadhehebu zimepandwa, na hivyo ndivyo mazao yangekuwa, na hivyo ndivyo yaliyo hasa.

213 Kaeni kimya kabisa. Kila mmoja wenu ni roho. Unaposogea. . . Bila shaka, kama wewe si roho, basi umekufa. Unaona? Roho inayochochea maisha yako, mdundo kutoka kwa roho, ndio hasa Yesu aliokuwa akizungumzia kuhusu yule mwanamke, alipowaona Mafarisayo, na kujua yaliyokuwa moyoni mwao, na angeweza kuwaambia; walikuwa wakifikiri

Yeye alikuwa ni Beelzebuli. Matabaka yote mawili daima yako karibu, daima yamekusanyika pamoja.

²¹⁴ Huyu hapa ameketi mwanamke, hapa mkono wangu wa kulia, akiomba. Anaomba kwa sababu ana uvimbe mgongoni mwake. Una kadi ya maombi? Huna. Huhitaji yoyote. Je, tunafahamiana? Hatufahamiani. Inua mkono wako ili watu waweze kuona. Hiyo ndiyo shida yako? Vema, mwamini Mungu, kitu hicho kitatoweka. Amina. Simjui, sijawahi kumwona, Mungu anajua hilo.

²¹⁵ Huyu hapa maskini mwanamke mmoja, ameketi papa hapa nje, amevaa nguo inayoonekana ya kijani kibichi, ameamisha kichwa chake, akiomba. Ana ugonjwa wa figo. Kama unaamini kwa moyo wako wote, Dada, Mungu atakuponya ugonjwa huo wa figo. Unaukubali? Je, una kadi ya maombi? Wewe, una moja? Huhitaji yoyote, ugonjwa wako wa figo ulikuacha.

²¹⁶ Nampa changamoto asiyeamini yeyote aniambie kile mwanamke huyo alichogusa. Kamwe hakunigusa, bali alimgusa yule Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Naam. Kama unaamini kwa moyo wako wote! Amina.

²¹⁷ Sasa, imeanza kusogea kila mahali. Huo weusi umeanza kurudi nyuma. Ulikuwa na kina sana hapa kwa dakika moja, lakini unarudi nyuma.

²¹⁸ Hapa ameketi mwanamke mbele yangu, anaugua mzio. Sikujui, Mama, lakini una mzio, sivyo? Unaamini ya kwamba Mungu anajua wewe ni nani? Kama ningetaja jina lako, kama Yesu alivyomwambia Simoni Petro, ungeniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Ungeniamini? Bibi Holt, amini kwa moyo wako wote, na uende nyumbani, na uwe mzima.

²¹⁹ Unaamini? Angalia. Iangalie. Hivi hamwezi kuiona hiyo Nuru? Angalieni hapa, iko moja kwa moja juu ya mtu anayeniangalia moja kwa moja, aliyeketi papa hapa nyuma.

²²⁰ Anaomba kwa ajili ya mke. Huyu ni wewe, Bwana. Una kadi ya maombi? Huna. Simama kwa miguu yako. Mke wake asipofanyiwa jambo fulani mara moja, atakufa, anaugua kansa. Hiyo ni kweli. Wewe hutoki hapa, umetoka mbali na hapa, unatoka kwenye mji unaoitwa Fresno. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu angeweza kuniambia wewe ni nani? Ingekusaidia kuamini? Ingekusaidia? Bw. Matthew, amini kwa moyo wako wote, rudi nyumbani.

²²¹ Ninampa changamoto asiyeamini yeyote, aniambie jinsi hilo linavyofanywa, nje ya nguvu za Mwenyezi Mungu. Unaamini hilo? Vema, usiogope, huyo ni Kristo, yale hasa Yeye aliyosema. Sasa, unaamini hilo?

²²² Sasa, ninawakabidhi kwa Kristo, ambaye yupo hapa. Kama utaamini kwa moyo wako wote, na kulikubali kwa misingi hiyo, unaweza kuponywa, umeponywa sasa hivi. Ni wangapi

wanaoamini hilo kwa mioyo yenu yote, bila ya kuwa na kitu kingine chochote, kwa ajili ya wokovu, kwa ajili ya uponyaji wako, utu wako wa kimwili, na utamwamini Mungu maishani mwako mwote, nawe utamkubali sasa hivi?

²²³ Uwepo Wake, ni Yeye, Kitu pekee kinachoweza kukusaidia, amini na usimame kwa miguu yako, useme, “Ninasimama sasa hivi, katika Jina la Yesu Kristo, kulikubali.” Kila mtu anayeamini, simama kwa miguu yako.

²²⁴ Wekeaneni mikono sasa, wekeaneni mikono. Biblia ilisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio,” kwa kuwa umekuwa mwaminio, kama wewe ni mwaminio sasa, Biblia ilisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa watapata afya.” Ni kama tu kutubu, na kubatizwa, ni kutii amri ya Mungu. Sasa, ombeaneni, jinsi tu mnavyoomba kanisani mwenu. Ombeaneni, ninapowaombea kutoka kwenye—kutoka kwenye jukwaa hili.

²²⁵ Baba wa Mbinguni, nimefanya haya yote kwa amri Yako, nimeyafanya jinsi tu ulivyosema yafanywe. Nami ninakuomba Wewe, Baba wa Mbinguni, kwamba katika Jina la Yesu Kristo, ya kwamba utaheshimu maombi ya watu hawa, imani yao, jitihada zao.

²²⁶ Shetani, umeshindwa vita, wewe ni kiumbe kilichoshindwa. Toka ndani ya watu hawa. Katika Jina la Yesu Kristo, waache, na utoke ndani yao.

Na mponywe kila mmoja. 

62-0629 Msiogope, Ni Mimi
National Guard Armory
Santa Maria, California Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org